



UKURASA 2

**ACT**: Siasa za uhasama hatari kwa Zanzibar




UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Februari 26, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581233

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Mafuriko CHADEMA yatikisa kwa Spika

UKURASA 2



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe, akihutubia wananchi wakati wa uzinduzi wa mikutano ya hadhara katika uwanja wa Ruanda Nzovwe jijini Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**



Rais mstaafu Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, akichangia mada kwenye mjadala wakati wa sherehe za maadhimisho ya miaka 20 ya Mpango wa Dharura wa Rais wa Kupambana na UKIMWI (PEPFAR), jijini Washington DC, Marekani juzi. Kulia ni Rais mstaafu wa Marekani, George W. Bush na Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani mstaafu, Dk. Condoleezza Rice. **PICHA: MPIGAPICHA MAALUM**

UKURASA WA 2

## NDUGU WA MAJERUHI AJALI YA MWENDOKASI HAWAJAJITOKEZA

NDUGU wa majeruhi wa ajali iliyohusisha basi la mwendokasi na gari dogo ambaye amelazwa Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU) kwenye Taasisi ya Tiba ya Mifupa...

UKURASA WA 4

MAKALA MAALUM

## MJUE MWANAJIOLOJIA WA KWANZA TANZANIA

WANAJIOSAYANSI nchini na kwingineko duniani wataikumbuka kwa majonzi tarehe 28 Desemba 2022, siku ambayo Tanzania ilimpoteza...

MAKALA MAALUM

# Dunia imechafuka na uanaume umetikiswa

UKURASA 5

## Kigogo wa CCM matatani madai kumjeruhi kwa jiwe kiongozi wa kanisa

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA YATAMBA KULINDA HESHIMA** UK. 24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mafuriko CHADEMA yatikisa jimboni kwa Spika Tulia

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAELFU ya wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) jana walifurika kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya kwa ajili ya kuwapokea viongozi wa kitaifa wa chama hicho.

Jijini Mbeya, ambako ni jimboni kwa Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kulishuhudiwa idadi kubwa ya wanachama na wafuasi wa chama hicho waliofurika kwa lengo la kuwalaki viongozi wa kitaifa walioongozwa na Mwenyekiti, Freeman Mbowe, wakitoka mkoani Songwe walikozindua mikutano ya hadhara juzi.

Katika uzinguzi wa mikutano hiyo kwa Mkoa wa Mbeya jana, chama hicho kilitoa rai mahususi kwa Jeshi la Polisi, kikilitaka kuacha kutekeleza amri zinazokiuka haki za binadamu ili kuepuka kulisababishia taifa machafuko.

Mwenyekiti wa chama hicho, Mbowe, ndiye aliyetoa rai hiyo kwa jeshi hilo, akidai kuwa katika kipindi cha miaka saba iliyopita, jeshi hilo lilikuwa linatumika kukandamiza uhuru wa siasa.

Mbowe alisema walikuwa hawawezi kufanya mkutano wa aina yoyote bila kuwapo kwa magari ya polisi wenye silaha na yale ya maji ya kuwasha, maarufu washawasha.

Alisema jukumu la Jeshi la Polisi kunapokuwa na mikutano ya kisiasa, ni kulinda hali ya usalama kwenye mikutano yote ya siasa bila kujali ukubwa wa chama husika.

"Kote tulikotoka wananchi wametupokea kwa kucheza, kukumbatiana na kuimba kwa shangwe na hapa Mbeya hilo limefanyika pia, ni kwa mara ya kwanza tunafanya mkutano bila gari la washawasha. Kwa hiyo, niwashauri askari wetu, msikubali amri za ovyo," alisema Mbowe.

Alisema ajenda ya chama hicho ni kuboresha mfumo wa utawala kwa kupunguza utitiri wa mikoa na kuiunda nchi kwa mfumo wa majimbo kama ambavyo nchi jirani ya Kenya inafanya.

Alisema kwa kufuata utaratibu wa aina hiyo, kila jimbo litakuwa na utaratibu wa kuwachagua viongozi wake na kuondoa utaratibu wa baadhi ya viongozi kuteuliwa na Rais na badala yake watachaguliwa na wananchi wa jimbo husika.

Alisema utaratibu huo unasaidia kuboresha usimamizi wa rasilimali za taifa kwa kurejesha utawala mikononi mwa wananchi wa eneo husika, badala ya kuchaguliwa viongozi ambao wakati mwingine wanakuwa hawawajui.

Alisema ili kufanikisha jambo hilo, Katiba ya nchi inatakiwa kurekebishwa ili viwapo vipengele ambavyo vinawapa wananchi haki.

"Tunataka katiba ambayo itarejesha madaraka kwa wananchi, wananchi wawe na uhuru wa kuchagua viongozi wao, tunataka katiba ambayo itawaondolea kinga viongozi wa serikali, zinawafanya wasishtakiwe wanapofanya makosa wakiwa madarakani," alisema.

Mbowe alieleza kuwa nchi inakabiliwa na matatizo mengi kwa sasa kutokana na alichokiita utawala usiofuata sheria na haki za binadamu, ikiwamo uminyaji wa demokrasia ya vyama vingi.

Alisema kwa sasa vijana wengi wanaohitimu elimu ya vyuo vikuu hawaajiriki kutokana na kile alichokiita sera mbovu ya elimu iliyopo ambayo haiwawezeshi kujiajiri.

Aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi, maarufu Sugu, alisema kuwa baada ya kuzuiwa kwa mikutano ya kisiasa, viongozi wa chama hicho walikuwa hawana sehemu ya kukutana na wananchi na kuzungumza mambo ya maendeleo zaidi ya kwenye misiba.

Alisema yeye ni miongoni mwa viongozi wa chama hicho walionyanyaswa kwa kufungwa gerezani kwa makosa ambayo alidai hayakuwa na ukweli.

Alidai kuwa baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, baadhi ya wafanyabiashara wa Jiji la Mbeya ambao walikuwa wanakiunga mkono chama hicho, waliporwa mali zao na baadhi walibambikwa kesi za jinai ikiwamo kuuza dawa za kulevya.

"Hivi karibuni, Rais alisema fedha zilizoporwa kwa wafanyabiashara hao zimewekwa kwenye akaunti za China, tunamtia moyo Rais atumie mbinu zote vikiwamo vyombo vya kimataifa kurejesha fedha hizo nchini, ili zitumike kuboresha huduma za kijamii," Sugu alisema.

Alisema baadhi ya miradi ambayo viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wanajinadi nayo jijini humo, ikiwamo barabara ya njia nne na mradi wa maji wa chanzo cha maji cha Kiwira, yeye ndiye alianza kupigania siku nyingi akiwa mbunge.

Alisema miradi hiyo aliipigania akiwa bungeni na aliwahi kuiomba kwa Rais John Magufuli alipofanya ziara jijini humo.

Sugu alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa serikali kuanza kutekeleza miradi hiyo ambayo itakuwa suluhu ya matatizo yanayowakabili wananchi na kwamba yeye ndiye aliyewashawishi watu kuvunja nyumba zao kwa hiyari.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA Taifa, John Heche alidai kwa sasa wananchi hawana watu sahihi wa kuwasemea kwenye Bunge kutokana na wabunge waliopo kuwa wa upande mmoja.

Alisema endapo wabunge wa CHADEMA wangekuwapo bungeni, baadhi ya mambo ambayo yanawaumiza wananchi yasingekuwa yanapitishwa kirahisi, likiwamo suala la kikokotoo cha mafao ya wastaafu na tozo za kwenye miamala ya simu.

Mwenyekiti wa chama hicho Kanda ya Nyasa, Mch. Peter Msigwa alidai CCM imeua mfumo wa elimu uliokuwa unawafanya vijana kufikiri na kwamba nchi inakabiliwa na matatizo mbalimbali kwenye sekta zote na hakuna michakato ya maana inayofanywa na serikali katika kuyatatua.

CHADEMA inaendelea kuzindua mikutano ya hadhara kwenye mikoa ya Kanda ya Nyasa ambapo leo itaizindua wilayani Rungwe na Mbarali kabla ya kwenda Njombe.

## Ndugu wa majeruhi ajali ya mwendokasi hawajajitokeza

**Na Romana Mallya**

NDUGU wa majeruhi wa ajali iliyohusisha basi la mwendokasi na gari dogo ambaye amelazwa Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU) kwenye Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) kwa siku nne sasa, hawajajitokeza.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Uhusiano wa MOI, Patrick Mvungi alibainisha kutokujitokeza kwa ndugu wa mgonjwa huyo ambaye afya yake inaendelea kuimarika.

"Majeruhi huyu bado yupo ICU na afya yake inaendelea kuimarika lakini ndugu zake mpaka sasa hawajajitokeza," alisema.

Ajali hiyo ilitokea Jumatano ya wiki hii eneo la Kisutu, ikihusisha gari ndogo aina ya Rav 4 lenye namba ya usajili T 978 DHZ na basi la mwendokasi lenye namba za usajili T 122 DGW.

Video fupi iliyorekodi tukio hilo lililotokea majira ya saa 12:31 asubuhi, ilionyesha namna ajali hiyo ilivyotokea kwa magari hayo kugongana, basi la mwendokasi likipoteza mwelekeo na kwenda kumgonga mwenda kwa miguu huyo, mwanamume aliyekuwa akipita maeneo hayo kisha kwenda kugonga ukuta wa maduka.

Wakati wa ajali hiyo basi la mwendokasi lilikuwa linatokea Kivukoni kuelekea Kimara na dereva wa gari dogo aliingia barabara ya mwendokasi bila kuchukua tahadhari, hivyo kusababisha ajali hiyo iliyowaacha watu 37 wakijeruhiwa.

# ACT: Siasa za uhasama ni hatari kwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama Cha ACT Wazalendo, Juma Duni Haji amesema Zanzibar inahitaji siasa za maridhiano na sio za uhasama ambazo zinachochea chuki na vurugu.

Amesema zama za siasa za uhasama zimepitwa na wakati na sasa wanahitaji kuijenga Zanzibar mpya, moja na yenye mamlaka kamili.

Aliyasema hayo jana visiwani Zanzibar wakati wa uzinduzi wa ahadi za chama hicho (brand promise), hafla iliyohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kisiasa kikiwamo Chama Cha Mapinduzi (CCM), viongozi wa dini na asasi za kiraia.

Alisema viongozi wa chama hicho wataendelea kudai maslahi ya Zanzibar katika Muungano wa Tanzania kwa sababu lazima uwe wa haki na kuheshimiana.

Alisema viongozi wa chama hicho wanastahiki kuaminiwa na Wazanzibar kuiongoza Zanzibar katika maridhiano ya kisiasa na kuiletea maendeleo.

Duni alisema ACT ni chama pekee kinachojitahidi kutekeleza utendaji wake kwa mujibu wa katiba ya chama hicho kwa kuwa na sera za hoja na kuikosoa serikali.

"Tutakapopewa dhamana ya kuiongoza Zanzibar, tutaiongoza vizuri na kuwaletea maendeleo wananchi," alisema.

Kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe alisema licha ya viongozi wa chama hicho kupigwa na kupewa ulemavu wa kudumu, linapokuja jambo la kukaa pamoja mezani kuijenga Zanzibar ya maridhiano, huwa wa mwanzo.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Othman Masoud Othman alisema Wazanzibar wanataka kuwa na Zanzibar yenye neema, mshikamano, baraka na maendeleo ili kufika safari wanayoitaka ya kuwa na mamlaka kamili.

"Maono yetu ACT tutakapopata ridhaa ya kuongoza dola, tunataka kuiacha Zanzibar mwaka 2035 kuwa Zanzibar mpya, moja na yenye mamlaka ambayo itakuwa na sera bora za kiuchumi, kijamii na uendeshaji wa nchi," alisema.

Pia alisema wanahitaji Zanzibar mpya yenye katiba mpya, mifumo bora ya mahakama na utoaji haki, iliyo madhubuti katika vita dhidi ya rushwa.

Kadhalika, alisema wanataka Zanzibar iliyoboresha huduma katika utumishi wa umma, mamlaka za serikali za mitaa na yenye miundombinu imara na ya kisasa inayopendezesha miji na kuifanya nchi kufanana na miji mikubwa duniani kama ilivyo Singapore, Hongkong na Dubai.

"Tunataka Zanzibar mpya yenye kuheshimu haki ya wananchi wake katika matumizi ya ardhi, ujenzi wa nyumba za gharama nafuu ambazo zitamwezesha kila mwananchi kumudu makazi ya kisasa, yenye watu wenye afya njema na mifumo bora ya huduma za kinga na matibabu pamoja na hifadhi ya jamii kwa wote.

"Tunataka nchi yenye kujitosheleza kwa nishati ya umeme wa uhakika isiyo na athari kwa mazingira na kutoa huduma bora ya maji safi na salama kwa watu wote mijini na vijijini," alisema.

Pia alisema wanatamani kuona Zanzibar mpya inayotoa elimu bora na bure mpaka chuo kikuu, inayozalisha vijana wenye maarifa na walioajiriwa kwenye shughuli za uzalishaji uchumi.

Pia alisema wanatamani nchi isiyo na ubaguzi katika nyanja zote, yenye umoja, haki, usawa, maridhiano na kuheshimiana.

Katibu wa Idara ya Itikadi, Uenezi na Habari wa CCM Zanzibar, Khamis Mbeto Khamis aliipongeza ACT na kusema kuwa Watanzania wanahitaji amani na utulivu, hivyo ni vyema kuheshimu haki za watu.

"CCM ipo tayari kukosolewa, ni vyema vyama vya siasa kufanya siasa za kistarabu na upendo kwa sababu Watanzania ni wamoja, vyama vinaweza kufa lakini nchi ikabakia," alisema.

Aliwataka viongozi wa vyama vya kisiasa kuendelea kuvumiliana na kuendelea kuwaletea maendeleo wananchi.

Alisema hakuna haja ya kulumbana kwa sababu Zanzibar itapata maendeleo wananchi wake wote wakiwa wamoja.

## HABARI KITAIFA

### Serikali yaja na mkakati kuongeza uwazi kiutendaji

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

IDARA ya Habari – MAELEZO na Ofisi ya Msemaji Mkuu wa Serikali iliyo chini ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, imeanza kuendesha mijadala ya mtandaoni ya CLUB HOUSE kupitia chaneli ya 'Maelezo News' na kundi mjadala la 'Msemaji Mkuu wa Serikali'.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Gerson Msigwa, Mkurugenzi wa Idara ya Habari – MAELEZO na Msemaji Mkuu wa Serikali, mijadala hiyo itakuwa ikirushwa kila Jumamosi kuanzia saa 3:00 usiku hadi 4:00 usiku ambapo mawaziri wakiwa na wataalamu wa wizara zao watakuwa wakishiriki kujadili mada mahususi zinazohusiana na sekta zilizo chini ya wizara zao na watajibu maswali ya papo kwa papo kutoka kwa wananchi, kupokea ushauri na malalamiko mbalimbali.

Jana walianza na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Moses Nnauye ambaye aliambatana na wataalamu wake katika mjadala kuhusu 'Utekelezaji wa Mradi wa Anwani za Makazi'.

Mijadala hiyp inaendeshwa ikiwa ni utekelezaji wa mkakati wa mawasiliano wa serikali unaolenga kushirikisha wananchi katika masuala mbalimbali yanayotekelezwa na serikali, kupanua uwazi na kufanyia kazi kero za wananchi kwa wakati.

"Nyote mnakaribishwa kushiriki kwa kutumia simu zenu za mkononi ama vishikwambi (tablets) kwa kujiunga na chaneli ya serikali ya 'Maelezo News' katika kundi la 'Msemaji Mkuu wa Serikali' ili muweze kusikiliza, kuuliza, kutoa maoni na kuhoji masuala mbalimbali yanayoihusu serikali," alisema Msigwa.

# Kigogo wa CCM matatani akidaiwa kumpiga jiwe kiongozi wa kanisa

**Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA**

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ameliagiza Jeshi la Polisi kumkamata Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Siuyu wilayani Ikungi, Said Daa anayetuhumiwa kumpiga jiwe na kumjeruhi kichwani Mchungaji wa Kanisa la EAGT, Kijiji cha Makotea.

Alitoa maagizo hayo jana wakati wa mkutano wa hadhara uliolenga kusikiliza kero za wananchi wa Wilaya ya Ikungi.

Katika mkutano huo, mchungaji wa kanisa hilo, Meshack Luya huku akionyesha jeraha kichwani, alimweleza Serukamba kwamba Januari 29 mwaka huu alijeruhiwa kwa kupigwa jiwe kichwani na mwenyekiti huyo wa CCM.

Alidai kwamba tukio hilo lilitokea majira ya saa nane mchana alipokwenda na waumini wenzake kwenye kiwanja kilichonunuliwa na kanisa na kwamba wana hati yake.

Alidai kuwa wakiwa eneo la tukio, ghafla alifika mwenyekiti huyo na kudai eneo hilo ni lake na kumpiga jiwe kichwani na kumjeruhi.

Alidai kuwa baada ya tukio hilo, alikwenda kutoa taarifa Kituo cha Polisi Mungaa na kupewa fomu ya matibabu (PF3) na kwenda kupata matibabu kwenye Hospitali Teule ya Makiungu.

Mchungaji huyo alidai kuwa tangu atoe taarifa polisi, mtuhumiwa huyo hajakamatwa, hali ambayo inampa shaka na wasiwasi kuhusu hali ya usalama wa maisha yake na familia yake.

Baada ya maelezo hayo, Mkuu wa Mkoa alimuuliza Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Ikungi (OCD), Suzan Kidiku kama anafahamu tukio hilo, alikiri kulifahamu.

"OCD hakikisha unamtafuta na kumkamata Mwenyekiti huyo wa CCM, haiwezekani mtuhumiwa asikamatwe tangu Januari 29, hivi kwa mfano mlalamikaji angekuwa amekufa mngefanyee?" alihoji.

Nipashe ilipomtafuta mtuhumiwa huyo, alidai mchungaji huyo na waumini wenzake walivamia eneo lake la shamba na kudai ni lao.

Hata hivyo, mtuhumiwa huyo alikanusha kumjeruhi mchungaji huyo kama ilivyoelezwa na kudai kuwa jeraha alilonalo mchungaji hajui alikolitoa wapi.

"Mimi sikumjeruhi huyo mchungaji, isipokuwa walipokuja yeye na wenzake kwenye eneo langu, wao ndio walinipiga na nilikwenda polisi kutoa taarifa," alidai.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Wailes, Manispaa ya Temeke, mkoani Dar es Salam, wakionyesha utaalamu wao wa kutengeneza sabuni mbele ya viongozi kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), walipoenda shuleni hapo jana, kufungua klabu ya ujasiriamali. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali, sekta binafsi kuzalisha wataalamu ufundi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika utoaji elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, ili kuzalisha wataalamu wenye ujuzi wa kutosha unaohitajika katika sekta mbalimbali.

Pia ametoa wito kwa waajiri kuendelea kushirikiana na serikali katika kuhakikisha malengo ya kukuza ujuzi na kuongeza soko la ajira yanafanikiwa kwa mustakabali wa maendeleo ya taifa.

Majaliwa aliyasema hayo juzi wakati wa hafla iliyokutanisha Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) na wadau ili kutambua mchango wa uzalishaji wa rasilimaliwatu yenye ubora kwa soko la ajira.

"Maendeleo ya uchumi wa nchi yoyote yanategemea sana ngazi ya ujuzi wa nguvukazi uliyonayo, hivyo mchango wa wadau ni muhimu," alisema.

Majaliwa aliwapongeza waajiri kwa kutoa nafasi za mafunzo kwa vitendo, uanagenzi, utarajali pamoja na namna wanavyoshiriki katika kuandaa mitaala inayotumika kwenye vyuo na taasisi za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

Alisema ushirikiano huo ni muhimu katika kuendeleza ujuzi kwa ajili ya kujenga uchumi wa viwanda.

"Serikali inatambua na ina thamini juhudi mnazozifanya katika utoaji wa ajira kwa wahitimu wetu, tunawapongeza," alisema.

Akizungumzia kaulimbiu ya mwaka huu inayosema 'Kuimarisha Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa Uzalishaji wa Wafanyakazi Wenye Ujuzi Nchini Tanzania', Majaliwa alisema inaweka msisitizo katika ujenzi wa rasilimali watu yenye ujuzi.

"Ni ukweli usiopingika bila ujuzi, hakuna maendeleo yoyote yanayoweza kupatikana, ujuzi unahitajika kwenye nyanja mbalimbali za uzalishaji, mataifa yote yaliyopiga hatua kubwa za maendeleo yamefanikiwa kwa kuweka kipaumbele katika kuongeza rasilimali watu yenye ujuzi," alibainisha.

Alitaja maeneo yaliyowekewa msisitizo ni sekta za kipaumbele, kuimarisha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu na kati ili kuhakikisha vijana wanaohitimu wanapata maarifa na ujuzi wa kazi utakaowawezesha kujiajiri na kuajirika.

"Hii ni pamoja na kuimarisha mifumo na kuongeza kasi ya kurasimisha ujuzi ili nguvukazi ya taifa itumike ipasavyo katika soko la ajira la ndani na nje," alisema.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda alisema serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uendelezaji wa Ujuzi wa Mwaka 2016/17-2025/26 ambao moja ya malengo yake ni kuwa na ushirikiano kati ya waajiri, wadau na vyuo au taasisi za elimu.

"Ushirikiano huu uteleta tija kubwa na kuondoa dhana ya kwamba wahitimu wetu hawana ujuzi unaohitajika katika ulimwengu wa kazi," alisema.

Mtendaji Mkuu wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Suzanne Ndomba-Doran alisema ili Tanzania iweze kushiriki kikamilifu katika soko shindani la Afrika Mashariki na dunia, ni lazima hatua za makusudi zichukuliwe katika kukuza ujuzi hususani kwa vijana.

"Katika kutimiza adhma hii, ATE tunaamini waajiri wana nafasi kubwa katika kufikia malengo tuliyojiwekea kama nchi.

"Mfano, kupitia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, awamu ya tatu, tumelenga kupunguza ukosefu wa ajira kutoka asilimia tisa (mwaka 2019) kufikia asilimia nane ifikapo mwaka 2025/26.

"Kukuza ujuzi ni kati ya mipango iliyobainishwa na serikali ili tufikie lengo na kuongeza idadi ya wahitimu waliopata mafunzo mahali pa kazi, hii ni njia mojawapo ya kukuza ujuzi nchini kwa vijana wetu," alisema.

Aliongeza kuwa wanatarajia kuongeza idadi ya wahitimu wenye mafunzo ya uanagenzi ili wafikie 231,000 ifikapo mwaka 2025/26 kutoka 46,000 mwaka 2019/20, vivyo hivyo na kwa mafunzo tarajari.

Alisema lengo ni kufikia wahitimu 150,000 ifikapo mwaka 2025/26 kutoka 30,000, mwaka 2019/20.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TANGA
Kituo cha MJINI TANGA Mkoa TANGA
Usimamizi wa mirathi na 42|2023
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU HASHIMU HASSANI
KATIKA SHAHURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI
YALIOLETWA NA SAUMU HASHIMU HASSANI

TANGAZO

(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama zamwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa

Hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 Mwezi 02 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa wa mirathi hiyo.

Zingatia;

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehem anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

Imetotewa leo tarehe 24 Mwezi 02 mwaka 2023

HAKIMU
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

LEVINA CLARA MAPULI anatangaza kupotea kwa kadi za gari zenye usajili namba: T402 BAG, T844 AYM ,T540 AVY, T738 AUQ. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/74046/2023

## RUMISHA HENRY KIMAMBO (1934 – 2022)

# Mjue mwanajiolojia wa kwanza Tanzania

## •Wanajiosayansi wamuenzi



WANAJIOSAYANSI nchini na kwingineko duniani wataikumbuka kwa majonzi tarehe 28 Desemba 2022, siku ambayo Tanzania ilimpoteza Rumisha Henry Kimambo, Mtanzania wa kwanza nchini kusomea taaluma ya miamba, Jiolojia.

Wanajiosayansi wa Tanzania wanamuenzi kama baba wa taaluma ya jiolojia nchini, mtangulizi aliyefanya kazi nyingi kwa utumishi uliotukuka.

Kimambo alizaliwa tarehe 15 Februari 1934 kwenye Kijiji cha Mbokomu, Wilaya ya Moshi Vijijini mkoani Kilimanjaro. Mwaka 1946 hadi 1950 alipata elimu ya msingi katika Shule ya Msingi Natiro-Mbokomu na baadaye elimu ya sekondari katika shule za Ilboru, Arusha na Tabora Boys, Tabora.

Mwaka 1958 hadi 1961, alisoma masomo ya sayansi katika Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda. Baada ya hapo, alijiunga na Chuo Kikuu cha Glasgow, Uingereza (Scotland) mwaka 1961 na kuhitimu Shahada ya Kwanza ya Sayansi ya Jiolojia (BSc.) mwaka 1965.

Kumbukumbu zinaonesha kuwa alikuwa ni Mtanzania wa kwanza kusoma na kutunukiwa BSc katika fani ya jiolojia na ni kwa msingi huo pamoja na kazi alizofanya, wanajiosayansi Tanzania wanaona anastahili kuitwa baba wa taaluma ya jiolojia Tanzania.

Mwaka 1965 mara baada ya kumaliza masomo Uingereza, Rumisha Kimambo alirejea nchini na kuajiriwa na serikali katika Idara ya Rasilimali Madini (inayojulikana sasa kama Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania - Geological Survey of Tanzania (GST)), ambayo wakati huo ilikuwa na waajiriwa wanajiolojia wa kigeni tu, hususan kutoka Uingereza ambao serikali iliwarithi kutoka serikali ya ukoloni baada ya kupata uhuru mwaka 1961.

Mara baada ya kuajiriwa alitumia muda mwingi katika miaka miwili ya mwanzo kufanya kazi za utafutaji wa madini na kuandaa ramani za jiolojia akiwa kwenye miradi iliyokuwa inafadhiliwa na shirika la Umoja wa Mataifa la UNDP iliyokuwa katika ukanda wa dhahabu wa Kanda ya Ziwa Victoria.

Chini ya miradi hiyo, madini ya dhahabu yalingunduliwa eneo linalojulikana kama Buckreef mkoani Geita mwaka 1966. Baada ya ugunduzi huo, utafiti wa kina ulifanyika na hatimaye Mgodi wa Dhahabu wa Buckreef ulijengwa na kuanza uzalishaji wa dhahabu mwaka 1984 ukiwa chini ya umiliki asilimia 100 kwa 100 wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO).

Mgodi huo ulifanya kazi kwa takriban miaka minane na kufungwa mwaka 1989/90 kutokana na matatizo ya kiufundi. Mgodi huo wa Buckreef ulianza tena uzalishaji mwaka 2020 na sasa unazalisha wastani wa wakia 2,000 za dhahabu kwa mwezi. Huu ni ushahidi hai wa ugunduzi uliofanywa na Rumisha Kimambo pamoja na timu yake.

Mwaka 1967 hadi 1969, Rumisha Kimambo alikwenda kusomea Shahada ya Uzamili ya Sayansi katika utafutaji wa madini katika Chuo Kikuu cha McGill kilichoko Montreal, Canada.

Baada ya kurejea nchini mwaka 1969, alipandishwa cheo na kuwa Mjiolojia Mkuu wa GST, nafasi aliyoitumikia hadi mwaka 1971. Mwaka 1972, aliteuliwa kuwa Kamishna Msaidizi wa Madini katika Wizara ya Biashara na Viwanda ambayo wakati huo ilikuwa inasimamia sekta ya madini na akahamishiwa Dar es Salaam kutoka Dodoma ambako ndiko kulikuwa na makao makuu ya wizara.

Baada ya kipindi kifupi kwenye wizara, mwaka 1972, Rais, Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, alimteua kuwa Meneja Mkuu ili kuliongoza Shirika la STAMICO lililokuwa limeanzishwa na kukabidhiwa migodi iliyokuwa inasimamiwa ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC).

Akiwa Meneja Mkuu wa STAMICO aliwezesha ukuaji mkubwa wa STAMICO ambayo ikawa na kampuni tanzu nyingi ikiwamo Mgodi wa Almasi wa Williamson Diamonds na kampuni zaTancutAlmasi, Tanzania Gemstone Industries, Tanzania Portland Cement (Wazo Hill), Nyanza Salt Mine, Pugu Kaolin na Tanganyika Meerschaum Corporation Ltd.

Bidii na ari yake kubwa ya kazi vilisababisha Mwalimu Julius Nyerere, mwaka 1976, kwa mara nyingine tena, kumteua kuwa Meneja Mkuu wa Shirika jipya la Tanzania Saruji Corporation (SARUJI). Shirika hili lilipewa jukumu la kuendeleza viwanda vya kutengeneza bidhaa zinazotokana na madini ambayo ni malighafi viwandani.

Akiwa Meneja Mkuu wa SARUJI, kiwanda cha Saruji cha Wazo Hill (Portland Cement Factory) kilipanuliwa na viwanda vipya vya saruji vya Tanga na Mbeya vilijengwa.

Aidha, katika kipindi chake, Shirika la SARUJI lilianzisha kampuni tanzu zifuatazo:- ni Mbagala Sheet Glass, Morogoro Ceramics, Nyanza Container Glass, Saruji Trucking na Saruji Training Institute.

Alistaafu kazi kutoka Shirika la SARUJI mwaka 2000 baada ya kampuni tanzu zilizounda Shirika la SARUJI kubinafsishwa. Baada ya hapo, aliendelea na shughuli zake binafsi katika fani ya ujuzi wake ya jiolojia.

Mzee Rumisha Kimambo pia atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa katika kuanzisha Idara ya Jiolojia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1974. Mafanikio yake mengine makubwa ni pamoja na kuwa mwasisi wa Jumuiya ya Wanajiolojia wa Tanzania (TGS) mwaka 1969 na kuwa Rais wake 1986.

Pia aliwahi kuwa Mwenyekiti na Mjumbe wa Bodi za mashirika mbalimbali ya umma na ya binafsi kama vile Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Kiwira Coal Mines Ltd, na Tanzania Portland Cement (Wazo Hill).

Eneo lingine ambalo Rumisha Kimambo alionyesha umahiri ni katika kuandika na kuchapisha vitabu vya kisayansi na jambo hili kwa kiasi kikubwa, ndilo linawafanya wanasayansi wa Tanzania na nje ya nchi kuendelea kumkumbuka.

Kwa mfano, atakumbukwa kwa juzuu zake mbili za vitabu kuhusu madini ya viwanda katika Tanzania. Juzuu hizo ni "Development of Non-Metallic Minerals and Silicate Industry in Tanzania Volume I - Basic Concepts, Strategies and Achievements " mwaka 1986 na "Development of Non-Metallic Minerals and the Silicate Industry in Tanzania Volume II - A profile of the Silicate Industry in Tanzania" mwaka 1988. Juzuu zote mbili zilichapishwa na kampuni ya uchapishaji ya East African Publications Ltd.

Kwa watu waliowahi kufanya kazi na Rumisha Kimambo wanamkumbuka kwa uongozi uliokuwa makini. Alikuwamtu msikivu, mwenye kuwajali wakubwa kwa wadogo. Wengi wanashuhudia kuwa alikuwa na uwezo mkubwa wa kupambanua mambo na kufikia uamuzi thabiti na mwafaka kwa hoja kinzani.

Kwa sasa wanajiosayansi wa Tanzania wanajadiliana kuhusu uanzishwaji wa Tuzo Maalum/zawadi kwa heshima ya jina lake. Pendekezo mojawapo ni kuanzisha nishani ya kila mwaka ya Rumisha Kimambo kwa mwanafunzi bora katika kozi ya Jiolojia katika mojawapo ya vyuo vikuu vya nchini.

Pendekezo lingine linahusu kuyapa jina lake madini mapya yatakayogunduliwa nchini siku zijazo ingawa hili linahitaji wanajiosayansi wa Tanzania kushirikiana na mashirika mengine ya kimataifa ambayo yana mamlaka kuhusu utoaji wa majina ya madini mapya yanayogunduliwa.

Taarifa hizi zimepatikana kutokana michango ya watu walioorodheshwa hapa chini. Shukrani za pekee zimwendee Prof. Sospeter Muhongo, Mbunge wa Musoma Vijijini ambaye pia ni Profesa mstaafu wa Jiolojia katika Idara ya Jiolojia ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Waziri wa zamani wa Nishati na Madini.

Sisi wanajiosayansi wa Tanzania tuna huzuni kubwa kwa kuondokewa na baba wa taaluma ya Jiolojia Tanzania. Hakika ameacha urithi unaopaswa kuzingatiwa na kila mwanajiosayansi. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. AMINA.

**Imeandaliwa na wanajiosayansi wafuatao:**
**Prof. Sospeter Muhongo,**
**Florian Ngunangwa,**
**Dk. Peter Dalaly Kafumu,**
**Dk. Athanas Macheyeki,**
**Julius Sarota,**
**Gideon Nasari,**
**Emmanuel Jengo na**
**George Mwakarukwa.**

# Dunia imechafuka, uanaume umetikiswa

## ●Ulaji, unywaji pombe sehemu ya tatizo
## ●Mikakati imeelekezwa kumwinua mwanamke

**Na John Mabula**

UANAUME umetikiswa! Ndivyo unavyoweza kusema kwa sasa kutokana na yale yanayoendelea katika jamii zetu tunamoishi.

Zamani ukikaa katika vilinge mkijadili uanaume, basi unapata picha za uanaume kuwa ni pamoja na urijali, kulea na kuhudumia familia, ukakamavu na nguvu nyingi.

Ujasiri na vitu kama hivyo ndivyo vilikuwa vinamtambulisha mtu kama mwanamume kamili. Lakini kadri siku zinavyokwenda, uanaume kamili umeanza kutikiswa na hata kuibuka majina ya ovyo dhidi ya wanaume.

Hivi sasa ni kawaida kusikia maneno kama 'mwanaume wa Dar', 'wanaume wa Kinondoni' na 'wanaume wa mikoani', yote haya yanalenga kuonesha mtikisiko unaowakumba wanaume siku hizi.

Kimsingi, uanaume umeanza kutikiswa na vitu vikubwa viwili - kwanza, tatizo la nguvu za kiume na la pili tabia chafu za mapenzi ya jinsia moja.

Bado sijakutana na utafiti wa kina kuhusu kiini cha tatizo la nguvu za kiume ambalo sasa linaonekana kuwa kubwa na limeshamiri zaidi tofauti na zamani, lakini mtindo wa maisha hususani ulaji wa vyakula, unatajwa sana kuwa ni moja ya visababishi vikuu.

Kwa mfano, ulaji wa vyakula vya mafuta mengi ambayo hupelekea shinikizo la damu au ugonjwa wa moyo, huathiri uzalishwaji wa nguvu za kiume. Uvutaji wa sigara na unywaji wa pombe kupita kiasi, ulaji usio makini unaosababisha uzito mkubwa, ulaji wa vyakula vyenye sukari nyingi, matumizi ya dawa zenye kemikali ni sehemu ya mzizi wa tatizo.

Vyote hivyo pamoja na vingine kadhaa visivyohusisha vyakula, hupelekea kwenye janga la upungufu wa nguvu za kiume.

Kwa upande mwingine, kuna hili janga la mapenzi ya jinsia moja, nalo linatajwa kuutikisa uanaume.

Sababu inayotajwa sana kuhusu kushamiri kwa uchafu huu ni kutokana na utandawazi, kwamba umesababisha vijana wetu waone na kusikia mambo mengi yanayoendelea duniani, yanayofaa na yasiyofaa ikiwamo suala hili la mapenzi ya jinsia moja ambalo awali lilikuwapo zaidi katika nchi za magharibi na huko linaonekana ni suala la kawaida kupitia mgongo wa wanachokisema wenyewe kuwa ni haki za binadamu.

Mtazamo wangu binafsi ni kuwa pamoja na utandawazi, kama nchi au dunia nzima kwa ujumla tumejikita zaidi na kuwekeza kwa mtoto wa kike na kumsahau kabisa mtoto wa kiume.

Kila unapopita kwenye majukwaa kuona kinacholengwa, unabaini ni kwa ajili ya mtoto wa kike, makongamano ni kuhusu mtoto wa kike, mikutano ni ya mtoto wa kike, ni nadra sana kusikia mtoto wa kiume akiwekewa uwanja wake na kuzungumzwa kwa mapana yake kuhusiana na hatari zinazomkabili.



Unywaji pombe  kupita kiasi ni moja ya tabia hatarishi zinazopunguza hadhi ya mwanamume.

Kwa mawazo yangu, hili linaweza kuwa kisababishi pia, kwa kuwa kijana wa kiume asiyefundishwa ubaya au athari za mapenzi ya jinsia moja, akikutana na mtu anayeyahusudu, basi ni rahisi sana kijana huyu kurubunika kwa sababu hajakutana na majukwaa yaliyomfungua akili kuhusu ubaya wa masuala hayo katika uzito wake kulinganisha na ukubwa wa tatizo hilo.

Ninafikiri serikali, wazazi na jamii kwa ujumla wabadili mtazamo na kuanza kumtupia jicho kijana wa kiume, maana mapenzi ya jinsia moja kwa wanaume yameanza kuonekana kama jambo la kawaida huku mitaani, ilhali ni janga kubwa linalopoteza vijana.

Ikumbukwe sheria za nchi yetu haziruhusu uchafu huu. Hata hivyo, kuona uhalisia wake, tembelea klabu za usiku maeneo ya Kinondoni na Sinza mkoani Dar es Salaam, utashangaa vijana wanavyojiachia waziwazi bila kificho, wakitumia majina ya aibu kama vile 'Aunt' bila kuwa na wasiwasi wowote.

Ni wazi dunia sasa imeshikwa na wanaoamini katika mambo hayo ya ovyo na wana nguvu kubwa za kiuchumi. katika hili ni vyema jamii kuwa macho na ushawishi wa kuwaingiza vijana katika uchafu huu.

Zipo sababu za kitaalamu zinazotajwa kusababisha uchafu huo, kubwa ikiwa ni kutowiana kwa homoni, yaani kijana wa kiume anakuwa na homoni nyingi za kike kuliko za kiume na ni sababu inayotibika kwa mtu anayegundulika hivyo.

Sababu nyingine inayosababisha uchafu huo ni tabia. Inaweza kuwa ni kwa kushawishiwa, kujaribu, kuiga au tamaa, hizi zote ni athari za kitabia.

Hapa ndipo wazazi tunapotakiwa kuamka. Zamani kutokana na mbanano wa shughuli zetu za kiuchumi, za kutafuta mkate wa kila siku, tuliachia jukumu la malezi kwa walimu na viongozi wa dini au kwa majirani na ndugu tuliowaamini huku tukiishi na msemo wa mtoto ni wa jamii yote.

Lakini angalia sasa hivi kote huko tulikokuwa tukikuamini ni kama nako kumechafuka. Hujasikia mtoto kalawitiwa na mwalimu wake? Hujasikia mtoto kalawitiwa na kiongozi wake wa dini? Hujasikia mtoto kalawitiwa na jirani yake? Hujasikia mtoto kalawitiwa na mjomba wake? Yote hayo yameshatokea na kuripotiwa. Je, watoto hawa wakizoea huo mchezo si ndio mazao mapya ya uchafu huo wa mapenzi ya jinsia moja?

Sijasema tusiwaamini tena makundi hayo niliyoyataja, ila ninachotaka kusema ni kwamba wazazi sasa tuondoke kwenye kivuli cha kuwa 'bize' na kazi, matukio hayo yawe filimbi vichwani mwetu kwamba tuna kitu cha ziada cha kufanya na hatua za kutakiwa kuchukua.

Kama wazazi tunatakiwa tuingie kwa miguu miwili kwenye usimamizi na malezi ya watoto wetu. Dunia imeshachafuka. Tutenge muda wa mara kwa mara kukaa na Watoto zetu na kuongea nao.

Kama una mtoto wa kiume, mwambie kwa uwazi sifa za mwanamume, mwambie uthamani wa uanaume wake, mwambie kama mwanamume akikua anatakiwa aoe kwa kuwa yeye ni mwanamume, mwambie kuwa mwanamume anaoa jinsia ya kike tu na jinsia ya kike inaolewa na jinsia ya kiume tu tofauti na hapo ni dhambi, uchafu na kujidhalilisha.

Tusiwafiche kitu, tuongee nao kwa uwazi na tujiweke karibu nao ili wawe huru kutueleza vishawishi au masaibu yao kama wanakumbana nayo huko mitaani. Tukijenga utamaduni huu, itawakaa kichwani na watakua navyo.

Nimesikia serikali imeanzisha mradi unaoitwa 'Timiza Malengo' ambao umeshaanza kufanya kazi katika mikoa mitano kwa kuanzia na lengo ni utapakae nchi nzima.

Ni mradi unaolenga vijana wa kike na wa kiume wa kati ya miaka 15-24, kuhusu elimu ya uzazi na Virusi vya Ukimwi. Rai yangu hili litumike pia kama jukwaa zuri la kuongea na vijana wa kiume kuhusu uchafu wa mapenzi ya jinsia moja, waelezwe kwa uwazi kuwa uchafu huo, kwamba ni kitu kisichokubalika.

Umri waliouchagua wa kuanzia miaka 15 ni sahihi kwa kuwa huku mitaani wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja, vijana wa umri kama huo ni wengi, japo kuna wa miaka 20, hivyo miaka 15 ni rahisi kumwahi na kumjenga.

Serikali pia inabidi iongeze ukali. Kwa mfano kuna tukio la kusambaa mitandaoni kwa picha za vitabu vinavyohamasisha mapenzi ya jinsia moja, unajiuliza vimeingiaje nchini Nani anavichapisha? Nani anavisambaza?

Hapa serikali lazima iwe na ukali kwa yeyote anayehusika navyo na ninashukuru kupitia kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Francis Michael, nimemsikia akikiri kuwa kuna shule zinazoingiza na kutumia vitabu vinavyohamasisha mapenzi ya jinsia moja, alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma hivi karibuni.

Sasa wameshajua hilo, kilichobaki ni kunyoosha makucha na kurarua wote waliobainika.

Lakini pia kumekuwapo madai ya kuwapo kwa vipindi vya katuni kwenye runinga vyenye viashiria vya kuhamasisha mapenzi ya jinsia moja, na tunafahamu watoto wanavyopenda katuni. Sasa nani anaruhusu maudhui ya aina hii kurushwa hewani nchini? Nani analifuatilia hili? TCRA si ya kwetu? Ichukue hatua.

Hapa pia rai yangu kwa wazazi, tuwe na udhibiti wa uangaliaji wa runinga kwa watoto wetu, tusiwaachie uhuru wa kuangalia muda wote bila usimamizi.

Uanaume umetikiswa kweli, lakini kwa pamoja tunaweza kuungana kuurejesha njia kuu ingawa inaweza isiwe kazi nyepesi kwa sababu inaonekana ni tatizo ambalo tayari lina mizizi mirefu.

Umoja ni nguvu, hapa ninazungumzia serikali na jamii yote kwa ujumla, wakiwamo wazazi, viongozi wa dini na walimu. Kwa pamoja tuchukue hatua ya kulizungumzia jambo hili kwa uwazi na kwa uzito mkubwa.

Kama nilivyosema awali kuwa nguvu ya ushawishi ni kubwa kutoka kwa hao walioushikilia uchumi wa dunia, lakini umaskini wetu usitufanye tuvunje tamaduni, mila na desturi zetu, tuungane na tuwapinge kwa nguvu zote ili tuwe na nguvukazi ya kiume iliyokamilika na kizazi cha kiume kilichostaarabika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tabia hizi za madereva bodaboda zikomeshwe

**USAFIRI** wa bodaboda kwa abiria umekuwa rahisi na tegemeo kwa muda mrefu nchini tangu uliporasimishwa. Mtu anapotaka kuwahi mahali fulani ama kwa shughuli za kibiashara, kikazi au mambo binafsi, usafiri anaoufikiria haraka ni pikipiki, maarufu kama bodaboda.

Sababu kubwa za kutumia usafiri huo ni kufika katika shughuli aliyoikusudia kwa wakati unaotakiwa tofauti na usafiri wa mabasi maarufu kama daladala au usafiri binafsi kwa wale waliojaliwa kuwa nao. Yote hiyo ni kuepuka usumbufu na msongamano wa magari barabarani na matokeo yake kushindwa kutimiza lengo lake kwa wakati mwafaka.

Tangu kurasimishwa zaidi ya miaka 10 iliyopita, usafiri wa bodaboda umekuwa maarufu sehemu mbalimbali nchini na ili uwe endelevu na wa kuaminika, Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani, limekuwa likisisitiza madereva kuheshimu sheria za usalama barabarani wakati wa kuendesha vyombo vyao ikiwamo kuvaa kofia ngumu wao na abiria wao na kuzingatia mambo yote kama ilivyo kwa madereva wa vyombo vingine vya moto.

Pamoja na kwamba ni usafiri rasmi na tegemeo kwa wananchi wengi, kumekuwa na kero nyingi ambazo zinasababishwa na madereva wa vyombo hivyo, zikiwamo kutofuata sheria za usalama barabarani, kuendesha kwa kasi na hata kuvuka taa za barabarani zikiwa katika alama nyekundu. Mbaya zaidi madereva wengi wamekuwa hawajijali kwa kutokuwa wasafi na kuvaa kandambili wakati wakiwa kazini.


Mbali na matatizo hayo, baadhi ya madereva wa bodaboda wamekuwa wakituhumiwa kushiriki katika matukio ya uvamizi na uporaji mali kwenye makazi ya watu na hata kujeruhi watu pindi wanapokumbana na upinzani dhidi ya watu wanaojihami. Kadhalika, wamekuwa wakidaiwa kupora simu na vitu mbalimbali ikiwamo mikoba ya kinamama wanaotembea kando ya barabara.

Licha ya matukio hayo, juzi katika halmashauri ya Chalinze, Bagamoyo mkoani Pwani, dereva wa bodaboda aliyekuwa anaendesha pikipiki iliyobeba magunia ya mkaa, alifariki dunia wakati wa vurugu zilizotokea eneo la Vigwaza, kwenye kizuizi cha Maliasili. Inadaiwa kuwa vurugu hizo zilikuwa kati ya wafanyabiashara wa mkaa wanaotumia bodaboda na walinzi wa kizuizi baada ya mmoja wao kukamatwa akitakiwa kulipa ushuru wa Sh. 50,000, kitendo ambacho hakuridhika nacho. Kutokana na kudaiwa kulipa ushuru huo, mmoja wa wafanyabiashara hao aligoma kulipa ushuru na kuwapigia wenzake ambao walifika mahali hapo kwa wingi ili waikomboe bodaboda hiyo iliyokamatwa. Kwa mujibu wa Jeshi la Polisi, watu hao wakiwa na silaha za jadi, walivamia kizuizi kwa lengo la kuipoka pikipiki hiyo na kuondoka naye.

Watu hao pia walijaribu kuipokonya silaha aliyokuwa anaitumia mlinzi kwa madai haifanyi kazi ndipo mlinzi huyo alipofyatua risasi kwa lengo la kujihami na hatimaye kumpata mmoja ambaye alifariki dunia. Kitendo kilihofanywa na badoboda hao si cha kiungwana na kinapaswa kukemewa na jamii yote ya wapenda amani na utulivu ndani ya Tanzania.

Hiyo haikuwa mara ya kwanza kwa vijana hao wa bodaboda kwa kuwa wamekuwa wakifanya hivyo hata pale mwenzao anapofanya makosa ya usalama barabarani ikiwamo kusababisha ajali na kuwakusanya wenzake kwa lengo la kujihami. Matokeo yake wamekuwa wakisababisha uharibifu wa vyombo vya moto licha ya kuwa chanzo ni mmoja wao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wanasiasa pinganeni kwa hoja mkiendeleza umoja

**UPINZANI** ni neno maarufu katika siasa na katika dunia lilianza miaka mingi katika nchi zilizoendelea ziliporuhusu mfumo wa vyama vingi. Kwa Tanzania na Afrika kwa ujumla, suala hili lilianza kuwa maarufu mwishoni mwa miaka ya 1980 na mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Hapo ndipo mfumo wa vyama vingi uliingia na suala hilo limeendelea kusikika kutokana na wanasiasa wa chama tawala na upinzani wanavyotofautiana.

Utofauti wa wanasiasa makundi hayo mawili, unatokana na sera, mitazamo, hoja na mengine yanayohusu siasa, na yamekuwa yakisababisha hata wakati mwingine kuwapo malumbano makubwa miongoni mwao.

Lakini kabla ya kuendelea ningerudi kidogo katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la pili (TUKI), ambayo inaelezea maana ya upinzani kuwa ni hali ya kupingana, kubishana au kukinzana.

Ndani ya mfumo wa vyama vingi, wanasiasa wamekuwa wakishambuliana kwa maneno makali, huku kila upande ukijiona kuwa ni bora kuliko mwingine.

Binafsi siamini kwamba upinzani ni kupinga kila kitu, siamini kama ndani ya CCM hakuna lolote la maana, pia siamini kuwa upande wa upinzani unapopinga jambo huwa hauna hoja ya maana.

Ninaamini kwamba kutofautiana katika mtazamo, hoja, sera ni jambo la kawaida ambalo linaweza kuwafanya wanasiasa wakajadili kile wanachotofautiana na mwisho wake wakaibuka na matokeo mazuri.

Lakini wanasiasa wakiendelea kushikilia msimamo wao kwa 'kushambuliana' kwa maneno, huku kila upande ukijiona ni bora kuliko mwingine, watakuwa hawasaidii katika juhudi za kujenga nchi.

Ni vyema wanasiasa wakaweka maslahi ya taifa mbele kuliko vyama vyao, kwani inaonekana wazi kuwa malumbano ambayo yamekuwa yakijitokeza yanatokana na kuweka mbele maslahi ya vyama badala ya nchi.

Ingependeza kama watakuwa tayari kukosoana na pia kukubali hoja za msingi badala ya kubishana, huku kila upande ukitaka kuonyesha umahiri wa kutukana au kuonyesha wanavyojua kuliko wengine. Inawezekana wapo wanasiasa au Watanzania wasio na vyama ambao wanaamini kwamba kuwa mpinzani ni kuwa mkorofi, mhuni, mpingaji na mambo yote yakiwamo ya maana.

Vilevile wapo wanaoamini mtu kuwa katika vyama vya upinzani ni adui wa chama tawala na kukataa kushirikiana, lakini ukweli ni kwamba kutofautiana kiitikadi, kimtazamo mambo mengine ya kisiasa, ni jambo la kawaida.

Ikumbukwe kuwa, Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa akihimiza umuhimu wa kuwa wamoja kama Watanzania, kwani anatambua kuwa nchi hii itajengwa na Watanzania wote bila kujali itikadi za kisiasa.

Rais ameruhusu kuwapo kwa mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, huku akiwataka wanachama wa CCM kujiandaa kukosolewa na vyama vya upinzani kwenye mikutano hiyo na kuwataka kutoa hoja badala ya 'kupayuka' majukwaani.

Kwa kauli hiyo, ni wazi kwamba CCM inayoiongoza, imekuja na mwelekeo wa maridhiano, ustahimilivu, mabadiliko na kuijenga upya nchi kwa kushirikiana bila kujali itikadi za vyama.

Anasisitiza kuwa CCM inapokosolewa, iangalie yale ya kweli na kuyachukua na kuyafanyia kazi, na kwamba yale ambayo si ya kweli, wanachama wayajibu kwa hoja, lakini kikubwa anahimiza ustahimilivu.

Ninaamini kwamba kwa maelekezo hayo ya Mwenyekiti wa CCM Taifa, wanachama wa CCM hawatawachukulia wapinzani kama maadui bali watavumiliana na kukosoana kwa lengo moja la kujenga nchi.

Lakini pia, upinzani sio uadui, sidhani kama kuna sababu ya msingi ya kugombana vyama vya upinzani vyenyewe au na chama tawala, kwani kufanya hivyo kunaweza kuwa sawa na kuishiwa sera.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Tuonyeshane upendo kwa vitendo



Pascal Mayalla

SAFU ya Kwa Maslahi ya Taifa, inazungumzia jambo lolote lenye maslahi kwa taifa liwe la kisiasa, kiuchumi au kijamii. Kwa vile sasa tumeingia kipindi cha Kwaresma, mfungo wa siku 40 kwa Wakristo na mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani unatarajiwa kuanza mwezi ujao, leo nimeona nizungumzie kidogo kuhusu upendo. Upendo huu ni ule wa kupendana kwa dhati na kuonyesha upendo kwa vitendo.

Japo Mungu alitoa Amri Kumi na kumpa Nabii Musa kule kwenye mlima Jangwa la Sinai, amri hizi hazifanani kwani amri kuu kuliko zote ni Upendo. "Mpende Bwana Mungu wako kwa akili zako zote, kwa nguvu zako zote na uwezo wako wote, mpende na jirani yako kama nafsi yako."

Kwa hiyo kipindi hiki cha Kwaresma na mwezi Mtukufu wa Ramadhani unaokuja, Watanzania tupendane. Si tu tuseme tunapendana kwa maneno bali tuonyeshane upendo wa dhati. Si upendo wa maneno "nakupenda" bali upendo wa matendo ya kuonyesha upendo.

Kabla sijaendelea, ningeomba sisi Watanzania wote, wakiwamo viongozi wetu wote, serikali yetu, vyama vyetu, taasisi zetu, mashirika yetu, kampuni zetu, viwanda vyetu, vikubwa vya uzalishaji bidhaa kwa machine hadi viwanda vidogo vya Mama Ntilie vya kusukuma chapati, maandazi na vitumbua, kuiga kitu kinachofanywa na kampuni ya Mafuta ya TotalEnergies ambayo kila mwaka, siku ya Sikukuu ya Wapendanao, huonyesha upendo kwa vitendo kwa wateja wake wanaofika kujaza mafuta kwenye vituo vyake kwa upendo wa vitendo na si upendo wa maneno.

Kila Valentine's Day, TotalEnergies hutoa zawadi za aina mbalimbali kwa wateja wake kuanzia kupunguza bei ya mafuta kwa punguzo maalum la Siku ya Wapendanao, na hugawa zawadi maalum ya kuonyesha upendo iwe ni ua jekundu la waridi na kutoa zawadi za chokoleti zikiendana na bahati nasibu ya mteja mwenye bahati kupewa zawadi yoyote ikiwemo 'offer' ya kula mlo wa jioni yeye na mwenzi wake kwenye hoteli ya nyota tano.

Hiki kitu kinachofanywa na kampuni hii kila mwaka, japo kwa jicho la juu juu ni kitu kidogo, ukilinganisha thamani ya zawadi hizo na ukubwa wa kampuni yenyewe ya TotalEnergies kwa hapa Tanzania, ina zaidi ya vituo 100 vilivyotapakaa nchi nzima na mafuta yake yana ubora wa hali ya juu kutokana na kuongezwa kiambata cha 'exellium' chenye kimeng'enyo kinachosafisha injini ya gari kwa kutumia mafuta kidogo na kutoa moshi kidogo hivyo kudumisha gari lako huku likitoa moshi kidogo ambao ni rafiki wa mazingira.

Ukiangalia kilichofanywa na kampuni hii, unaweza kuona ni kitu cha kawaida na kusema ni vijizawadi tu. Lakini kiukweli ni kwamba zawadi hizo thamani yake ni kubwa na zimetolewa kutokana na tendo la kuonyesha upendo kwa vitendo na si kwa maneno matupu ya "nakupenda".

Upendo wa kweli haupimwi kwa thamani ya zawadi bali kwa matendo ya kuonyeshea ndiyo maana wenzetu wazungu mtu kuonyeshwa upendo kwa kupigwa busu, kupewa zawadi ya ua au kadi ya Valentine. Kwao upendo huo una thamani kubwa kuliko hata mtu akipewa mamilioni ya fedha. Japo kwa Kiafrika, kutokana na umasikini uliotopea, ili mtu ajione anapendwa ni pale akipewa fedha, sio busu, sio ua, sio kadi.

Umuhimu wa upendo ni upendo huo uwe ni upendo wa dhati wa kutoka moyoni na kuonyeshea kwa vitendo, ndiyo maana nimesema kinachofanywa na TotalEnergies kiigwe na wote.

Sasa turejee kwenye ile amri yetu Kuu ya Mungu ya upendo aliyopewa Musa. Japo duniani tuna dini mbalimbali na madhehebu mbalimbali, Mungu ni mmoja tu kwa dini zote na kwa dini kuu mbili za Wakristo na Waislamu, si wote wanafahamu Mungu wa Wakristo na Waislamu ni Mungu mmoja na amri za Mungu kwa dini zote mbili ni amri moja za Musa na Wakristo na Waislamu ni watoto wa baba mmoja Nabii Ibrahim.

Ibrahim na mkewe Sarah, hawakujaaliwa kupata mtoto mpaka wanazeeka, hivyo Sarah akamwomba mjakazi wake wa Kimisri Hagir, kumpatia uzao Ibrahim, hivyo mtoto wa kwanza wa Ibrahim aliitwa Ismail ndio uzao wa Waislamu mpaka Mtume Mohamed (SAW) na baadaye Sarah akajaaliwa mtoto Isaka ambaye ndiye uzao wa Wakristo mpaka Yesu aitwaye Kristo. Hivyo amri Kuu ya Mungu ya upendo ni ya wote.

Kwenye Kwaresma hii na Mwezi Mtukufu wa Ramadhani Watanzania, si tu tupendane bali tuonyeshane upendo wa kweli wa ishara na matendo ya upendo wa dhati kwa kumpenda jirani yako kama nafsi yako.

Je, jirani yako ni nani?. Jirani yako ni mtu anayekuhusu aliye karibu na wewe. Jirani wa jirani wa serikali ni wananchi, jirani wa viongozi ni wanao waongoza, jirani wa CCM ni vyama vya upinzani, jirani wa mfanyabiashara yoyote ni wateja wake.

Kama kila Mtanzania, serikali, kila kiongozi, kila taasisi na kila mtu atampenda jirani yake kwa upendo wa dhati na kuuonyesha kwa matendo, Tanzania yote itakuwa imejaa upendo wa ajabu. Mtashangaa hata vitendo vya uhalifu vitapungua!

Wafayabiashara hawatapandisha bei za vyakula Mwezi Mtukufu, vyama vya siasa, CCM na wapinzani, watapendana na kuoyesha upendo. Tutaijenga Tanzania njema yeye upendo, amani, utulivu, masikilizano, maelewano na kupata maendeleo ya kweli na maendeleo endelevu.

**Mungu ibariki Tanzania**
**Kwaresma Njema.**
**Paskali 0754 270403**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tusikurupuke kuamua bila kutafakari matokeo



Na Joseph Kulangwa

MUNGU alipoumba mbingu na nchi aliweka viumbe hai kwa maana ya binadamu, wanyama, wadudu, ndege na mimea na kumtaka binadamu aende kuvitawala.

Katika kundi la wanyama na ndege, wakiwamo wafugwao na wa porini. Kwa wanyama wafugwao wakawamo ng'ombe, mbuzi, kondoo, ngamia, punda, mbwa, paka na nguruwe.

Kwa upande wa ndege tukawa na kuku, bata, bata mzinga, njiwa na kasuku lakini wanyama pori wakawa ni wa aina nyingi sana kuanzia walao majani na walao nyama, waliwao na wasioliwa na binadamu.

Hali kadhalika kwa ndege wakawapo waishio porini, waliwao na wasioliwa. Samaki wakaendelea kuishi mitoni, maziwani na baharini. Lakini kwa tamaa ya binadamu kuwatawala, polepole akaanza kufuga hata wasiofugika, tukasikia na kuona fisi, mamba wakifugwa na baadaye samaki.

Haikushangaza pia kuona binadamu akifuga ngedere hata kama hakuliwa, akifuga nyoka na kuwatumia kuchezea ngoma kama ilivyokuwa kwa baadhi ya fisi ambao pamoja na bundi, walihusishwa na uchawi.

Lilikuwa jambo la kushangaza, kusikia binadamu amehamishia wanyamapori nyumbani na kuishi nao kwani ilizoeleka kuwa wanyama pori jamii ya paka walao nyama, ni hatari kwa maisha ya binadamu.

Hivyo wanyama pori wakabaki porini na kwenda kuwaona au kuwawinda mara moja moja. Hatimaye nchi zenye wanyama wengi wa porini, zikatenga maeneo ya kuhifawadhia na kuyaita hifadhi, mbuga au mapori tengefu.

Huko wakienda watalii kuwatazama na kulipa fedha za kigeni kwa ajili ya uchumi wa Taifa husika lenye hifadhi hizo za wanyama pori. Wapo walioruhusiwa kuwasogeza wanyama hao karibu na kujenga mazizi (zoo).

Kwenye mazizi hayo, nako waliruhusiwa watalii wa ndani na nje kwenda kuwatazama kwa malipo. Ndipo pia baadhi walichukuliwa na kupelekwa kwenye mabanda maalumu ya maonesho, na kuruhusu watazamaji kuwaona kwa malipo.

Baada ya mazoea hayo, hivi sasa kumeibuka mazizi ambako kuna wanyama wa aina mbalimbali walao nyama na walao majani, ambako wanafungiwa na kulishwa badala ya kuwinda wenyewe, tabia ambayo si yao.

Kwa hali hiyo, hivi sasa wanyama hao wakiwamo wakali kama simba, kwa kutowinda na badala yake kulishwa kwa mikono, wamekuwa wapole kiasi cha kuweza kukaa sehemu moja na binadamu kama akaavyo na paka au mbwa.

Kwa kifupi, hivi sasa wapo simba wa kufugwa, chui wa kufugwa, tembo wa kufugwa, nyati na hata pundamilia wa kufugwa, wakaao na binadamu karibu na ingewezekana hata wangekuwa wanapeana soga.

Muktadha huo, umefanya hata binadamu aweze kumshika simba mkia na asimfanye lolote, kwa kuamini kwamba hatamfanya lolote, ili mradi anapata haki yake ya shibe na hivyo kujenga urafiki na binadamu.

Inasahaulika lakini, kwamba mnyama ni mnyama tu iko siku anaweza kubadilika akasababisha maafa makubwa kwa binadamu, kwa kukosa uvumilivu achokozwapo na ndipo mfugaji atageuzwa chakula na mfugo wake.

Kinachoendelea pale Mbezi Luis kwenye stendi ya John Magufuli, nakifananisha na hali hii ambapo hivi sasa kuna mjadala unaendelea wa tozo za viingilio vya abiria katika stendi hiyo kubwa nchini.

Awali, viingilio vilitozwa kwa wasio abiria huku abiria wenye tiketi wakiruhusiwa kuingia kwa tiketi zao kwa kuamini kwamba katika nauli walizolipia kupanda mabasi yatokayo hapo, tozo hiyo inakatwa.

Lakini kutokana na vikao ambavyo inashangaza vilifikiaje uamuzi huo, abiria hata walio na tiketi wanatakiwa kulipa viingilio hivyo na kujikuta wakilipa mara mbili, na hiyo ni mbali na kulipia vyoo wanapobanwa.

Ni dhahiri kuwa serikali yoyote inayotaka kuboresha maisha ya watu wake, huboresha miundombinu ya huduma, ikiwa ni pamoja na hospitali, barabara, shule na stendi kama hizo, kwa kujua pia kuwa wananchi wake wanalipa kodi kupitia maeneo mbalimbali.

Lakini sasa tofauti ni kuwa miundombinu ikijengwa, watumiaji ambao ni wananchi wanatozwa huduma kana kwamba inamilikiwa na wageni; hiyo ni pamoja na madaraja na stendi kama hizo!

Najiuliza, mbona tuendapo kwenye viwanja vya ndege tukiwa tayari tumelipia tiketi za safari hatutozwi viingilio wala huduma za vyoo? Kwa nini wahusika wanapoulizwa baada ya kupitisha, kusimamia utekelezaji wa uamuzi, ndipo hujifaragua kwa kauli za tunashughulikia? Huwa wanaamua wasichokijua au? Msione wanyama wanakubali kushikwashikwa, kuna siku watachoka! Alamsiki!

**(kulangwasos@gmail.com)**

# MATUKIO KATIKA PICHA




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako (katikati), akiwa ameshika kitabu cha 'On My Father's Wings' kilichoandikwa na Mwanzilishi wa shirika la ndege la Precision Air, Michael Shirima (wa tatu kushoto), baada ya kukizindua jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wengine ni Zahid Mustafa (kushoto), Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo (wa pili kushoto), Jenerali mstaafu Mrisho Sarakikya (wa tatu kulia) Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba (wa pili kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mhandisi Peter Lusekelo (kushoto), alipotembelea kiwanda cha kutengeneza kadi za benki na NIDA, akiwa katika ziara ya kukagua na kusikiliza changamoto za wenye viwanda jijini Tanga mapema wiki hii. Wa (pili kulia) ni Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Rashid Liemba. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**



Waziri Mkuu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Sensa ya Watu na Makazi, Kassim Majaliwa akizungumza wakati akifungua kikao cha Kamati hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**



Mafundi wakipanga mawe ili kujenga kingo za barabara ya mabasi yaendayo haraka inayoendelea kujengwa kutoka Gerezani hadi Mbagala, katika eneo la Bandari mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Shughuli za wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga zinasababisha takataka wanazozalisha kutupwa kwenye mtaro wa maji ya mvua katika Barabara ya Morogoro, eneo la Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, kitendo ambacho ni uchafuzi wa mazingira. **PICHA: SABATO KASIKA**


# MAISHA

FEBRUARI 26, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 15

## Hizi ndizo mbinu za kupambana na mchwa kwenye nyumba




Ukurasa 14

## BIRIANI YA SAMAKI




## KATUNIKA


Ukurasa 16



# WEKA USO UNAOVUTIA

Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | C | I | T | A | B | O | T | I | O | T |
| P | S | F | G | E | C | L | L | I | O | U |
| O | F | H | J | L | A | X | H | J | R | P |
| P | V | C | Z | N | Y | U | K | I | N | K |
| O | N | Y | K | I | E | B | P | O | D | S |


| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| B | U | U | ■ | P | A | A |
| A | ■ | ■ | W | A | ■ | C |
| N | ■ | V | ■ | N | ■ | H |
| D | A | I | ■ | G | O | A |
| A | ■ | M | ■ | A | ■ | N |
| M | ■ | B | I | ■ | ■ | G |
| A | R | A | ■ | M | K | E |

## AMSHA AKILI


Watoto wapendwa, msaidieni rafiki yenu Tau kutafuta njia ili apate vitabu vyake!



## TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

ITV, LOA, TRA, NAE, BAA, BAI, TAI, OGO, IKATE, BINGO, VUMILIA, TAMBIKO

## WATOTO

# PAKA RANGI







MAMA yake John alikuwa anafanya usafi chumbani kwake, ghafla alipokuwa akisafisha chini ya uvungu wa kitanda alikutana na kisanduku ndani yake kulikuwa na mawe 10.

Mama: We John kisanduku hiki cha nini?

John: Nilikuwa nayahesabu mayai ya kuku

Mama: Mayai ya kuku ndio haya mawe?

John: Hapana, mawe yalikuwa idadi ya mayai niliyoiba bandani na kuyala

Mama: Wee mtoto nitakuadhibu.

**SWALI**

Mbuga ya Taifa ya wanyama ya Nyerere ilikuwa ikitambulika kwa jina gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Migogoro ya ndoa inavyoathiri mwelekeo maisha ya watoto

KARIBU msomaji wangu tuendelee na mada zetu za Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki iliyopita nilijadili laana ya kuacha mke wa kwanza inavyotesa wanaume walio wengi. Nikasema wapo wanaume wanaodhani kuacha mke wa kwanza na kuoa mwingine ataishi kwa raha kumbe ni karaha tupu.

Sisemi ni wote wanakumbana na karaha, la hasha! Wako wanaopata ahueni pengine mke yule alikuwa na mapungufu mengi aliyoshindwa kuyamudu. Wengine wanafurahia maisha kwani misukosuko hupungua kama siyo kuisha kabisa.

Sasa leo hebu nigusie watoto wanaojikuta katika mazingira ya wazazi wenye migogoro katika ndoa. Je, malezi na makuzi yao yatakuwa salama? Picha wanayoiona kwa wazazi wao itawajenga kifikra na kisaikolojia katika maisha yao ya baadaye?

Wako wazazi wanaozozana wakirushiana maneno mazito huku watoto wakisikia na kuona kwa macho jinsi baba na mama wanavyodundana. Tena watoto wengine ni wadogo, jambo ambalo huwatia hofu. Kwa mantiki hiyo, unadhani watoto hawa watawaelewaje wazazi wao?

Katika hali ya kawaida ilipaswa wazazi wanapoingia kwenye mzozo fulani nyumbani kwao, yafaa waingie chumbani wakaulizane huko badala ya kupurukshana mbele za watoto.

Hiyo ni ili kuwasaidia hao watoto. Tukumbuke kwamba watoto ni wa taifa na malezi huanzia pale nyumbani. Ni mke au ni mume wa mtu unayemlea tangu mtoto. Kile unachomfundisha utotoni ni picha ya maisha yake baadaye.

Kila anachokiona mzazi akifanya, huamini ni kitu sahihi naye anaweza kukifanya baadaye katika maisha yake. Aliona baba akivuta sigara, naye kwa kificho akawa anavuta. Akija kuwa mvutaji sigara ukamgombeza, ataweza kukukumbusha, mbona wewe baba ulikuwa unavuta sigara? Je, hapo utakuwa na jibu? Alichokiona kwako ndicho atakifanya kama hukumjenga vema kimalezi.

Aliona wazazi wakipigana kila mara, naye atajiaminisha kuwa atakapokuwa na mke huko baadaye akimletea za kuleta atamdunda. Baba alikuwa na tabia ya wizi hata watoto kuwa wanasikia taarifa hizo mitaani. Roho ya wizi ikiendelea kwa watoto wake atamlaumu nani?

Nakumbuka upo wakati nilimtembelea mama yangu mdogo pale Kiboriloni Moshi. Kulikuwa na familia jirani ambayo baba na watoto wake wanne akiwamo mmoja wa kike, wote walikuwa wezi. Wanaiba hata mchana, ukiacha sufuria, kijiko nje hukikuti.

Nilipodadisi kumbe watoto hawa kazi hiyo ya wizi anayo baba yao, nao wakaamini kuwa ni sahihi hata wakiifanya hakuna shida. Kumbe ni hatari tupu. Siyo hivyo tu, hata maneno yale wanayotamka wazazi wakati wanazozana mbele ya watoto, huwa ni mbegu mbaya sana kwa maisha yao. Maneno ni nguvu.Hili nitalijadili wiki ijayo.

Wako watoto wanaosikia maneno mazito kutoka kwenye vinywa vya wazazi wao wakiamini ni maneno mazuri kumbe ni matusi mabaya. Sasa wanapoyatamka wakiwa wanacheza na watoto wenzao, na hata watu wengine wazima wakiyasikia wanabaki midomo wazi.

Wakiulizwa husema, si baba na mama nilisikia wakisema? Mtoto mdogo wakati wote awe anacheza, anakula na kadhalika huwa yuko anajifunza. Ndiyo maana wana maswali mengi wakitaka kujua hili na lile.

Hivyo wazazi wanapaswa kuwa makini na kuwasaidia kujua mambo mazuri na siyo mabaya yatakayoharibu maisha yao ya baadaye. Wanapaswa kuwa na staha mbele za watoto wao. Yapo maisha wanayoishi watu leo, chimbuko likiwa ni malezi mabovu ya wazazi wao tokea wakiwa wadogo.

Angalia jeshi la watoto wa mitaani, wengine wakiwa wamejazana katika vituo vya kulelea watoto yatima. Wakieleza historia ya maisha yao utajichokea mwili na roho.

Wengine watakuambia baba na mama walikuwa wakipigana kila wakati, nikaamua kutoroka nyumbani. Mwingine mama alikimbia baba akaoa mke mwingine lakini mama huyu wa kambo akawa ananitesa nikatorokea mjini kutafuta maisha.

Wako watu leo wanateseka kumbe ni kutokana na misingi mibaya iliyoasisiwa na wazazi, mababu na mabibi au hata koo zao. Wengi tunasahau kwamba kile tunachokitengeneza mwanzo, ndicho tutakikuta mwishoni, kiwe kizuri au kibaya. Maisha Ndivyo Yalivyo!

Uliyotarajia yatokee huyaoni kumbe zipo sababu za ndani na nje. Yawezekana zinatokana na wewe mwenyewe au na wazazi wako. Hutoboi kwa kila ukifanyacho kumbe mahali fulani iko shida.

***Hili nitajadili zaidi siku zijazo. Una kisa? Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Saa zahesabika kishindo kashfa ya ulawiti shuleni

TANGU serikali iliposhtuka kuhusu kashfa ya ulawiti shuleni, kumekuwa na hekaheka nyingi za viongozi wa serikali kupishana huku na huko wakikemea uchafu huo na wengine wakiweka hadharani misimamo yao.

Sakata hili la madai ya ulawiti na matukio mengine ya ukatili wa kingono, limeenda mbali zaidi na sasa huko mkoani Kilimanjaro, inaripotiwa kwamba tayari baadhi ya halmashauri zimeanza kuchukua hatua.

Moja ya halmashauri zilizoanza kuchukua hatua ni ya wilaya ya Moshi, iliyotangaza marufuku ya walimu wa shule za umma, kuvaa suruali za jeans shuleni, walimu wa kike kuvaa nguo fupi na za kubana mwili kuanzia Machi Mosi, mwaka huu.

Aidha, halmashauri hiyo imetangaza marufuku ya matumizi ya mavazi ya vibamba, kuvaa viatu bila soksi, wanaume kushona suruali za kubana 'hips' ili flaizi isifunge. Wanaamini hizo ni sehemu za dalili za wanafunzi kuingia katika uchafu unaotajwa wa ushoga na ulawiti.

Tunasahau kwamba wazazi na walezi wanapaswa kutafakari juu ya kupunguza harakati za kutafuta maisha, badala yake wawafuatilie watoto wao kuhusu dalili za ulawiti na ukatili dhidi ya watoto.

Najiuliza kabla ya kufichuliwa kwa kashfa hii walikuwa wapi? Walikuwa hawajui kuhusu haya au ulikuwa woga wa nani aanze? Kula! kura, zinawafanya wanasiasa wetu kujizima data kana kwamba walikuwa eti hawayaoni haya? Siamini hata kidogo.

Juzi, nimemsikia Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Chriss Makere, akihamasisha walimu wakuu wa shule za msingi na sekondari mkoani Kilimanjaro, kuanzisha vitengo vya intelijensia ya wanafunzi shuleni pamoja na madawati ya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto. Lengo la Afande Makere ni kupanua wigo wa kupambana na tishio la ukatili wa kijinsia na vita dhidi ya ulawiti.

Inapendeza kwa ujio huo wa mbinu mpya za kuukabili ulawiti na ukatili mwingine wa kingono dhidi ya wanafunzi shuleni. Natamani Jeshi la Polisi kupitia Kitengo cha Polisi cha Ushirikishwaji Jamii na Dawati la Jinsia, lingeingia kazini kuwapika wanafunzi watakaoteuliwa kwa siri na walimu wao kuwa kikosi kazi cha intelijensia shuleni.

> **Kwa kuwa intelijensia inahusika zaidi na ukusanyaji na uchakataji wa taarifa mbalimbali, vikosi kazi vya wanafunzi vinavyounda intelijensia shuleni, ni vyema vikafundwa kuhusu usiri na namna ya kujiheshimu.**

Nendeni mkawapige msasa, kwa kuwapatia mafunzo maalum ya namna ya kufuatilia nyendo za wenzao shuleni, walimu wao na namna ya kuwaripoti kwa usiri kwa 'mwalimu' ambaye atakuwa ameteuliwa kusimamia jukumu hilo ili kugundua mienendo ya wanafunzi na walimu wao.

Kwa kuwa intelijensia inahusika zaidi na ukusanyaji na uchakataji wa taarifa mbalimbali, vikosi kazi vya wanafunzi vinavyounda intelijensia shuleni, ni vyema vikafundwa kuhusu usiri na namna ya kujiheshimu.

Aidha, uwekwe utaratibu kwa wanaoteuliwa kufanya kazi hiyo wasijuane na wafundwe namna ya kufanya tathmini ya taarifa za kiintelijensia zinazohusu uadilifu wa wenzao, wakiongozwa na mwalimu maalum anayepokea taarifa hizo. Mwalimu huyo maalum, afundwe pia namna ya kuzichakata taarifa hizo kabla ya kuwasilisha ripoti yake kwa mwalimu mkuu wa shule ya msingi au mkuu wa shule ya sekondari ili kuchukua hatua.

Hatua si kufukuza shule kwa haraka, si kupiga, si kudhalilisha bali ni kukaa na mwanafunzi anayeonekana kutumbukia katika uchafu huo na kumdodosa alikopata mafunzo, alikoshawishika na nani alimfanyia ukatili huo ili kupata uhalali sasa wa kumwondoa kwa manufaa ya wengi au kumnusuru anayeonekana kuathiriwa na hali hiyo.

Tangu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, Januari 17, mwaka huu, alipounda tume maalum ya kuchunguza madai hayo katika mkoa wa Kilimanjaro, nimekuwa nikijipa kazi ya kufuatilia mienendo ya viongozi mbalimbali waliojitwisha ajenda ya kueleza athari za ulawiti.

Hii ni vita na mataifa mengi duniani yasiyokubaliana na ushoga na hasa Tanzania. Tunaisubiri kwa hamu ripoti ya Tume ya Kamishna wa Elimu nchini na wajumbe wake, Mwanasheria wa Wizara husika na Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora wa Elimu. Ninaposema saa zahesabika kishindo cha kashfa ya ulawiti shuleni, sijakosea, tuvute subira!

***Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com Simu ya mkononi: +255 767 535490***









Unaweza kuepuka gharama kwa kuipendezesha harusi kwa kutumia mavazi ya kitamaduni. Katika picha tofauti ni baadhi ya harusi zilizopambwa kwa mavazi ya kiasili.

# MITINDO





## ZINATAMBA MPAKA SASA

UNAWEZA kusema kwamba dunia ya mitindo ilianzia Ugiriki, lakini ukweli nchi hiyo ndiyo inayoitwa mama wa mitindo yote ya mavazi.

Katika makasri ya kifalme na familia za kitajiri ulimwenguni, mitindo maarufu ya mavazi wanayotumia basi inatoka Ugiriki. Unaweza kusema nchi hiyo sawa na bustani ya mavazi yanayopendwa na watu maarufu.

Hii inatokana na ukweli kwamba aina ya magauni yote yenye umaarufu chanzo chake inatoka nchi hiyo.

Unapowaona wanawake waking'ara kutokana na magauni yao marefu, yenye mitindo ya kushangaza, basi kumbuka kwamba asili yake ni kutoka nchi hiyo ya Ulaya.

Zipo nguo ambazo zina shingo za singo za V, au sehemu kubwa ya mabegani kuwa wazi, hiyo ni mitindo ya Kigiriki ya kale ambayo bado inapendwa hadi sasa.

Jamii ya Kigiriki ya kale walitaka kuwaona wanawake wana asili ya urembo, ndio maana hata nguo zao zilishonwa katika ustadi mkubwa ambao unaweza kueleza vyema kuanzia tumboni, shingoni hadi kichwani.

Hata aina ya viatu vinavyovaliwa sasa ni matokeo ya wabunifu wa kale ambao kila wakati walitaka kuona mwanamke yupo sawa na Malaika kutokana na mvuto wake.

UREMBO

Na Mary Geofrey

# WEKA USO UNAOVUTIA
## Madhara ya kutumbua chunusi





CHUNUSI ni vipele vinavyoota usoni, mgongoni na kifuani, kutokana na mabadiliko ya mfumo wa homoni mwilini.

Hali hiyo husababishwa na kutengenezwa mafuta mengi kwenye ngozi na hivyo matundu ya vinyweleo vya ngozi kuziba.

Kutumbua chunusi na vipele ni tabia ya watu wengi ambayo inaleta athari ya makovu, wekundu na kusambaza bakteria.

Japokuwa ni ngumu kutotumbua chunusi, fanya yafuatayo kila unapofikiria kutumbua chunusi.

Kama ulikuwa hujui ndio ujue kuanzia leo, kwamba chunusi inayotumbuliwa inaacha kovu na madoa meusi ambayo huchukua muda kuondoka, kuliko ile isiyotumbuliwa ambayo kovu au doa lake huchukua muda mfupi kupotea.

Kuchelewa kupona

Ukitumbua chunusi unachelewesha uponyaji na kwa sababu hiyo ngozi yako huchelewa kupona na kubaki na makovu.

Unasambaza bakteria na ndio maana ukitumbua chunusi moja leo, kesho unapata nyingine unatumbua tena na unabaki na makovu na chunusi zisizoisha! Usitumbue chunusi.

**Njia ya kuacha kutumbua chunusi**

Usipende kushika shika uso wako.

Ukiwa unajishika shika utapata hamasa ya kujitumbua chunusi.

Acha kujiangalia kwenye kioo na kuona wewe pekee ndie uliebarikiwa chunusi nyingi zaidi.

Wewe utaona una machunusi mengi na wala hakuna anaeshughulika nazo. Jifunze kujikubali.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# BIRIANI YA SAMAKI



BIRIANI ni aina ya wali ambao unapikwa kwa kuungwa na viongo mbalimbali.

Wengi tumezoea kupika biriani la nyama, kuku na mbizi, hivyo leo tunaelekezana kupika biriani la samaki.

Mchele kilo moja, samaki kilo moja, vitunguu kilo moja, samli robo, au mafuta ya kupikia, kitunguu saumu kiasi, mdalasini kiasi, hiliki kiasi, ndimu kiasi, tungule na chumvi kiasi.

**JINSI YA KUANDAA**

Mkate samaki umtie chumvi na ndimu umkaange. Menya vitunguu uvikate, saga tungule, saumu na viungo vyote vilivyobakia.

Injika sufuria utie samli, ikichemka tia vitunguu uvikaange, vikianza kupiga wekundu tia tungule na viungo kidogo.

Acha vikaangike kwa muda, halafu tia vipande vya samaki, chumvi na ndimu, pamoja na maji kidogo. Acha ichemke kwa muda mfupi na ikibaki rojorojo epua.

Chukua sufuria nyingine uitie maji na chumvi, yakichemka osha mchele utie, acha utokote.

Angalia kiini cha wali, ukiona umeshaiva umimine uyachuje maji yote. Bandika tena sufuria utie samli kidogo, ikichemka tia vitunguu kidogo pamoja na vile vilivyobakia.

Vyote vikaange kidogo halafu umimine wali wote ukoroge koroge ili upate kuchanganyika na viungo na halafu uweke vizuri upalie moto.

Ukishakauka utaupakua. Kuupakua kwake kwanza utatia wali kwenye sahani, baadae ndio utatia samaki pamoja na rojo rojo lake lote kwa juu.

MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Hizi ndizo mbinu za kupambana na mchwa kwenye nyumba

LEO tunajifunza namna ya kupambana na mchwa baada ya ujenzi wa nyumba.

Mdudu huyu amekuwa tishio kubwa katika ustawi wa nyumba na husababisha uharibifu mkubwa asipodhibitiwa.

Ziko mbinu mbalimbali za kupambana na mchwa huyo baada ya kujenga nyumba ambazo zinatajwa na mtaalam Leonard Chacha.

Chacha anasema namna ya kudhibiti mchwa kwenye nyumba baada ya ujenzi kabla ya kuanza kuitumia ni lazima yote inyunyiziwe dawa ili kuua mazalia yote ya mdudu huyo.

Anasema kudhibiti mdudu huyo wakati tayari unaitumia nyumba kunaweza kuleta usumbufu kidogo tofauti na ilivyo kwa nyumba ambayo haijaanza kutumika.

Anashauri kwamba ni vema mtumiaji au mmiliki wa nyumba kuweka utaratibu na mazoea ya kuweka dawa kila baada ya muda fulani kupita.

"Kabla ya kutumia dawa hizi za kuilinda nyumba yako dhidi ya mchwa ni vema ukapata ushauri wa mtaalamu wa ujenzi au kilimo na mifugo, kuna aina nyingi za dawa zinazotumika kwa sasa na bado nyingine zinaendelea kubuniwa kuendana na ukuaji wa sayansi na teknolojia ya utengenezaji wa dawa.

"Ni vema kutumia dawa kwa kuzingatia maelekezo ya mtaalamu au mzalishaji wa dawa hizo kwa sababu hazifanani katika mbinu za matumizi, hivyo usiige tu kutoka kwa wengine, ni vema kupata kwanza ushauri," anasema.

Anaelekeza kwamba kabla ya kuweka dawa kwenye nyumba, unapaswa kusafisha mifereji na kuhakikisha kwamba hakuna bomba zinazovuja ikiwamo kukausha maeneo yote yenye unyevunyevu.

Pia anasema kuweka dawa kwenye maeneo yote ambayo ni njia au makazi ya mchwa, na ambayo ni chanzo hata kama hakuna mchwa wanaoonekana.

Lingine anasema ni kung'oa na kuondoa mbao zote zilizoharibiwa na mchwa na kuweka nyingine pamoja na kutoruhusu mbao zozote zigusane na udongo wowote au unyevunyevu kwa muda mrefu na kuziba matundu yote kwenye sakafu na kuta.



## Namna ya kupamba kwa batiki, ukili



MVUTO wa chumba au sebule unaweza kuletwa kwa mapambo ya kienyeji rahisi, nafuu na kuonekana cha kisasa sana.

Baadhi ya mapambo haya ni yanayotengenezwa kwa malighafi za asili kutoka kwenye eneo ulilopo na ukaleta upekee wa nyumba.

Wataalam wa mapambo ya ndani wanaeleza kwamba mapambo ya ndani ya asili yanaleta lugha ya tofauti ndani ya nyumba na mawasiliano mazuri kwa wageni.

Jambo la kuzingatiwa katika mapambo ya asili kwa mujibu wa wataalam ni kuweka picha sehemu ambayo 'macho' yanapita kwa urahisi.

Miongoni mwa mapambo ya asili yanayotajwa na wataalam hao ni visahani vilivyofumwa kwa nyuzi nene zilizopangiliwa rangi au ukili ulionakshiwa kwa rangi.

Wanaeleza kuwa batiki iliyopangiliwa vizuri inaweza pia kutumika kuleta nakshi maridhawa ya asili.

Wataalam hao wanaeleza kuwa ukuta unaopanga kuweka pambo lako la asili unapaswa kuuandaa uonekane kama eneo la maonyesho ya kazi za sanaa.


Kitu kingine cha kuzingatia ni mpangilio wa mapambo kulingana na rangi. Inashauriwa kuweka rangi angavu au zilizopoa zinazoelekeana.

Wanaeleza kuwa pambo la asili ni rafiki wa mazingira kwa kuwa linatumia malighafi rahisi zilizopo eneo husika.

Wataalam wanaeleza kuwa mapambo ya asili yanaweza kutengenezwa kwa miundo tofauti tofauti mingi na kamwe hayachuji wala kupungua thamani.

Wanafafanua zaidi kwamba mapambo ya asili ya sanaa za nguo na ukili yametumika karne nyingi na fasheni isiyoisha mvuto ambayo yanapatikana kwa gharama nzuri.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
LILE SOMO LA KUTUNGA SENTESI NILILICHUKIA BURE! SASA NAONA UMUHIMU WAKE, NIKIULIZWA "UMEZIPATAJE?" NGOMA INAANZIA HAPO!
'FEDHWA'
DORALI
MIJI'MALI
ULE WIMBO ULIOIMBWA WANAUME TUMEUMBWA MATESO UNANIKUNA!
ZAWADI ZA 'SMOLU HAUSI'
BUZA
KAMA MIMI NIMECHUKULIWA MKE KISHA NIKA-MSAMEHE MGONI INAKUUMA NINI?
KINACHONIUMA SIO KUMSAMEHE, ILA KUMUACHA MGONI BILA KIDONDA 'ATAKUKUMBUKAJE?'
WE' BHANA TATIZO SIJAKUJUA KAMA 'KANDA MAALUMU' LISINGENTOKA NENO BAYA!
MNAWONA WOTE KWENE DARADARA NI WASARAMO SIO? REWO UTANIJUWA!
ONA RANGI YAKO INAVYOKIMBIZA WATEJA UPO KAMA MZIMU!
MWENYE RANGI YA KUVUTIA MBONA HAWAKAI UNA MIBA?
BAR
KIMWANA NAZALILIKA NA SUTI YANGU HUKU VICHOCHORONI SABABU YA MAPENZI
NDIO MAANA NAKUPITISHA HUKU WASIONE NIMEISHIWA NIMELIKAMATA 'JITU ZIMA'
*KINYUNYIZO CHA LEO...
MWENYE ZAMU YA UMEME KAJA NA MSHUMAA...

## HABARI KIMATAIFA



Wananchi wa Nigeria wakiwa katika foleni ya kuingia katika chumba cha kupiga kura jijini Logos, jana. **PICHA**: **AFP**

# Ukraine yatanda makombora, Zelensky aomba mazungumzo

**KYIV,** UKRAINE

Wakati Russia ikifanya mashambulizi ya anga kila kona nchini Ukraine, Rais Volodymyr Zelensky, amepanga kufanya mazungumzo na China ya namna ya kumaliza vita.

Kuanzia alfajiri ya jana, anga la Ukraine lilikuwa limetanda makombora na kusababisha watu kukaa kwenye mahandaki kwa ajili ya kunusuru maisha yao.

Kulingana na wavuti rasmi unaowapasha habari raia wa nchi hiyo, iliwanukuu maofisa wa Ukaraine wakisema kwamba Russia imeongeza mara dufu idadi ya meli zake za kivita katika Bahari nyeusi.

Taarifa kutoka jeshi la nchi hiyo, ilieleza meli nane za kijeshi zipo kwa sasa baharini, zikiwa zimebeba zana za kivita na makombora ya aina ya Caliber.

Kamanda wa Majeshi ya Ukraine, alisema huenda hali hiyo inaashiria maandalizi ya shambulio jipya dhidi ya nchi yao.

Wakati huo huo, Rais Zelensky, alisema anapanga kukutana na kiongozi wa China Xi Jinping, kujadiliana naye kuhusu mapendekezo ya namna ya kumalizika vita nchini Ukraine.

Akizungumza katika maadhimisho ya kwanza ya uvamizi kamili wa Russia nchini kwake, Zelensky alisema pendekezo linaonyesha kuwa Uchina inajihusisha katika kutafuta amani.

"Kusema kweli ninataka kuamini kwamba China haitaipatia silaha Russia,"alisema.

Mpango wa amani wa China unatoa wito wa kuwepo kwa mazungumzo ya amani na kuheshimu hadhi ya taifa.

Hatahivyo, waraka wa pendekezo hilo wenye vipengele vinne hausemi lolote kwa Russia inapaswa kuondoa wanajeshi wake Ukraine.

Maofisa nchini China bado hadi sasa hawajajibu wito wa Rais Zelensky wa kutaka mkutano na Xi.

Hata hivyo, Russia ilisifu mapendekezo ya amani ya China, ikisema kuna mitizamo inayofanana na taifa hilo.

Katika taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje, ilieleza wanakaribisha wazo la China la kuitisha mazungumzo yanayolenga kusimamia haki.

Aidha, Mkutano wa G20 umeshindwa kupata utatuzi juu ya masuala ya fedha na benki,kutokana na mitazamo tofauti ya nchi wanachama kuhusu vita vya Ukraine.

Waziri wa Fedha wa Marekani Janet Yellen, alisema anaamini taarifa ya mwisho ya kikao hicho lazima iwe ya kulaani vita vinavyoendeshwa na Russia.

"Tumefanya hili katika nyakati za nyuma, katika Bali, na hili ndilo ninaloliangalia kama jambo muhimu sana," alisema Janet Yellen.

Kauli yake inakuja huku kukiwa na uwezekano wa kutokubaliana katika maeneo yanayopaswa kuandikwa katika kauli ya mwisho ya kikao hicho.

India, ambayo ni mwenyekiti wa G20,inasisitiza kuhusu umuhimu wa kuondoa neno ''vita'' katika taarifa ya mwisho, kama walivyoliambia shirika la habari la Reuters.

Serikali ya India imekuwa na msimamo wa kutokuwa na mafungamano na upande wowote kuhusu vita, huku ikiongeza ununuzi wa mafuta yake kutoka Russia.

**BBC**

# Raia Nigeria wapiga kura, Bola, Abubakar wachuana vikali

**ABUJA,** NIGERIA

RAIA wa Nigeria wamepiga kura katika uchaguzi wenye ushindani mkali wa urais tangu kumalizika kwa utawala wa kijeshi.

Tangu mwaka 1999, nchi hiyo maarufu barani Afrika imekuwa ikitawaliwa na vyama viwili, chama tawala cha APC na kile cha upinzani cha PDP.

Lakini mwaka huu, kuna mgombea wa tatu kutoka chama cha Labour, Peter Obi, ambaye anaungwa mkono na vijana wengi.

Rais wa sasa wa Nigeria, Muhammadu Buhari, hagombei kiti hicho baada ya kuhudumu kwa mihula miwili.

Chama chake cha All Progressives Congress (APC), kinampeperusha mgombea wake ambaye ni gavana wa zamani wa Lagos, Bola Tinubu.

Makamu wa rais wa zamani Atiku Abubakar, anawania kiti hicho kwa kupitia chama kikuu cha upinzani cha Peoples Democratic Party (PDP).

Katika nafasi ya uraisi kuna jumla ya wagombea 18 .

Katika kampeni za uchaguzi zilitawaliwa na kauli zinazopinga uhaba wa fedha uliosababishwa na jaribio la kubadilisha sarafu ya nchi hiyo na kusababisha benki na machine za kutoa na kuweka pesa kuzidiwa.

Siku moja kabla ya uchaguzi mbunge wa Bunge la wawakilishi alikamatwa akiwa na pesa taslimu dola za Marekani,500,000 kwa ajili ya kuwahonga wapiga kura.

Yeyote atakayeshinda itabidi ashughulikie uundwaji mpya wa sarafu, kuyumba kwa uchumi, ukosefu wa hali ya juu wa ajira kwa vijana, na ukosefu wa usalama ambao umesababisha vifo vya watu 10,000 mwaka jana.

Uchaguzi wa mwaka huu umewavutia wapiga kura wengi wanaopiga kura kwa mara ya kwanza pamoja na vijana ambao ni theluthi ya watu milioni 87 wenye uwezo wa kupiga kura.

Obi (61)anatarajia kuvunja mfumo wa vyama vikuu viwili baada ya kujiunga na chama cha Labour Party mwezi Mei mwaka jana.

Ingawa alikuwa katika chama cha PDP kabla ya hapo, anaonekana kama sura mpya na ana uungaji mkono miongoni mwa baadhi ya vijana wa Nigeria.

Mfanyabiashara huyo Tajiri alihudumu kama gavana wa jimbo la kusini-magharibi la Anambra,kuanzia mwaka

Watu wengi wanachukulia uchaguzi huo kama kura ya maamuzi kwa chama cha APC, ambacho kimekaa madarakani katika kipindi cha hali ngumu ya uchumi na kuzorota kwa usalama.

Mgombea wake, Bola Ahmed Tinubu, 70, alisifiwa kwa kujenga mji wa kibiashara wa Nigeria Lagos, wakati wa mihula yake miwili kama gavana hadi mwaka 2007.

Anafahamika kama baba wa siasa katika kanda ya kusini- magharibi, ambako amejivunia ushawishi mkubwa, lakini sawa na Abubakar, amekuwa akikabiliwa na madai ya ufisadi. **BBC**

MAKALA

# MAFANIKIO YENYE HUZUNI NA MAJUTO



Na Magabilo Masambu

MAFANIKIO yoyote katika maisha ni mchakato mrefu. Jambo zuri tu ni kwamba tumepewa haki na nafasi sawa katika kuyatafuta mafanikio yenyewe. Kwa hiyo uamuzi unasalia kwetu ama tuutafute au tusubiri kutazama wengine wakifanikiwa.

Mafanikio ya watu wengi mara nyingi yamekuwa siri kubwa. Wako wanaoonekana kufanya shughuli fulani lakini shughuli hiyo si ndiyo imewapatia mafanikio hayo. Si rahisi kwa wenye mafanikio makubwa kusema ukweli juu ya njia walizozitumia kuyafikia.

Mathalani, unaweza kumwona mtu ni kiongozi fulani na amefanikiwa sana ukadhani uongozi umempatia mafanikio, kumbe ndani yake kuna wizi wa mali za umma, rasilimali za nchi, uhujumu uchumi au aina nyingine yoyote ambayo si picha ya nje watu wanayoifahamu.

Wako watu wanafanikiwa kwa kuumiza wengine. Wako wanaoteuliwa kwenye nafasi za madaraka kwa sababu wamewachongea wengine na kusababisha wafukuzwe kazi ili nafasi hizo zichukuliwe na wao. Wako walioua ili wapate mali za marehemu na wamefanikiwa kuzipata. Wengine wametuhumiwa kuua mpaka ndugu zao wa karibu ili wabaki na mali.

Wako wanaotuhumiwa na wengine kuthibitika kuua mpaka wenza wao baada ya kuona wamefanikiwa ili mali wabaki nazo lakini wakati tunazungumza haya, wengine wanawaza kufanya hivyo sasa. Wengine wamedhulumu mali za wajane, wamebaki wanahangaika ili wao wafanikiwe. Hivi ni kweli damu za watu zimekuwa rahisi kuliko mali zao tunazochukua? Unajisikiaje kama wewe ni miongoni mwa waliotenda uovu huu ili ufanikiwe?

Ni ukweli kwamba mafanikio ya haki yanachukua muda mrefu lakini ni bora ukachukua muda mrefu ukapata mafanikio yasiyo na majuto wala huzuni. Huzuni na majuto huleta mfadhaiko wa moyo, yaani unakuwa na mali za kila namna lakini kila ukikumbuka namna ulivyozipata, furaha ya moyo inaondoka. Unabaki na furaha ya machoni tu ili kuwafanya watu wasigundue.

Wengi waliofanikiwa kwa namna hii mwisho wao huwa si mzuri. Presha na sukari zinazowapata wengi zinatokana na msongo wa mawazo kwa sababu ndani ya mioyo yao wanafahamu madhambi yaliyowapatia mali hizo. Tukifikiria kupata mali za haki uovu na uhalifu juu ya binafamu na wanyama utapungua sana.

Kama ni vyeo tusubiri tuvipate kwa haki, kwa sababu kipimo unachotumia kumpimia mwenzako ndicho utakachopimiwa pia. Kama ni polisi acha tabia ya kubambikizia watu kesi ili ufanikiwe haraka. Utafanikiwa lakini utaandamwa na matatizo lukuki katika maisha yako au ya ndugu zako kwa sababu wako watu mali wanazipata kwa jasho na damu halafu wewe unatumia mavazi ya umma kuwanyang'anya!.

Kama ni daktari usiumize wagonjwa kwa kutaka upewe rushwa ndiyo utoe huduma na kwamba kama rushwa haipo basi na kufa afe, halafu akishakufa utajisikiaje maisha yako yote kila ukikumbuka kwamba ulikuwa sehemu ya kifo hicho? Kwa vyovyote damu hiyo itakulilia na hautabaki salama japo ni vigumu kujua namna malipo ya jambo hilo yatakavyokuwa. Hali kadhalika, kama ni hakimu usifunge watu kwa sababu unakula rushwa ili ujenge mapema. Unanunua maumivu ya kudumu bure.

Tusitumie nafasi zetu kuumiza watu ili tuyapate mafanikio mbalimbali kwa sababu ziko njia sahihi tu za kuyapata. Riziki ya mtu huwa haichukuliwi ila inaweza kuhifadhiwa kwa muda tu. Nafasi kama si yako, utaondolewa kwa kutumia njia zile zile ulizotumia kuwaondoa wengine.

Tafsiri yake ni kwamba kama ulipata nafasi yoyote kwa hila, utaondolewa kwa hila zile zile, ni suala la muda tu haujafika kwa sababu ukiua kwa upanga utauawa kwa upanga. Inawezekana ukasema hiyo ni imani tu, sawa lakini nakwambia inafanya kazi maana apandacho mtu ndicho avunacho. Ukipanda wema utavuna wema na ukipanda ubaya utavuna ubaya vilevile.

Kuna aina nyingine ya watu kazi yao kubwa ni kushiriki kukwamisha mafanikio na maendeleo ya wengine. Hii inatokana na hofu ya kutojiamini. Kila unayemwona unahisi atachukua kazi yako au ataua biashara yangu. Hofu hiyo huzaa uovu ambao unasababisha kuangamiza wengine ili kuendelea kulinda nafasi yako. Lakini upande wa pili na wewe ukipata nafasi sehemu tulia. Umekaribishwa sebuleni unataka kuingia mpaka chumbani kwa mama mkwe? Matokeo yake unaanza fitna, majungu mpaka unahakikisha umemwondoa aliyekukaribisha. Je, hayo mafanikio utakayoyapata kupitia nafasi hiyo utayafurahia?

Hakuna raha yoyote ya kuwa na mali zenye huzuni na majuto. Kila mtu anayo kanuni ya maisha yake. Usijilinganishe maisha yako na wengine japo unaweza kujifunza wanafanyaje. Usitake mashindano ya maisha kwani hakuna aliyewahi kushinda kwa sababu kila mmoja ana wakati wake wa kufanikiwa. Tatizo ni kwamba, wanaoanza kazi leo wanajilinganisha na waliokaa katika kazi zaidi ya miaka 20. Usiendeshwe na hisia za wengine.

Ndoa nyingi zimeingia kwenye migogoro kutokana na kujilinganisha. Jirani yako anatoka na gari nzuri asubuhi unaanza mbona wale wana nyumba wana magari sisi hatuna kwa nini? Je, wamekwambia wameyapataje?

Ukiambiwa njia walizotumia utaziweza? Unataka uwe na mali huku ukiwa mwenye huzuni na majuto muda wote uko tayari? Tukiacha kujilinganisha, badala yake tujifunze basi tutapata mafanikio ya haki na yenye furaha japo yanaweza yasiwe makubwa lakini tuna amani.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Mshenga mbabaifu aliyeingia mitini na posa, akiiacha harusi njia panda*



Na Adam Fungamwango

MSHENGA ni mtu anayeagizwa kupeleka barua ya posa nyumbani kwa binti ambaye amempendeza mwanamume fulani, hivyo kutaka kuwa wake wa maisha. Utamaduni huu umerithiwa tangu enzi na enzi, hadi leo hii.

Kabla Waafrika hawajajua kusoma na kuandika, mshenga alitumwa kuwasilisha wazo lililotolewa na anayetaka kuoa pamoja na familia yake.

Anakwenda kwenye familia ya binti na kupeleka ombi kutoka kwenye familia ya mwanamume. Tena akienda huko haendi kusema “familia ya fulani inataka kumuoa fulani, la hasha.”

Kwa wazee wa zamani hilo ni kosa kubwa na mke hupati. Kuna maneno ambayo yanatakiwa yazungumzwe ambayo yatawafanya wazazi wa binti kufahamu nini kinatakiwa bila kuwa na lugha ambayo wao walikuwa wanaona ya ukakasi. Mshenga anaweza kusema hivi “Wazazi nimekuja hapa kuiwakilisha familia ya fulani. Tumeona ua zuri limechanua. Tunaomba ruhusa yenu tulichume, tulipeleke kwenye familia hiyo ili likaendelee kumwagiliwa na kupaliliwa.”

Maneno hayo tosha yaliwafanya wazazi kutambua nini kinazungumzwa. Na kama ni nyumba yenye wasichana wengi au wanaofuatana umri, mshenga anaweza kuulizwa ni yupi ambaye wanamhitaji.

Ilipokuja enzi ambazo Waafrika walianza kujua kusoma na kuandika, kuna kitu kiliongezeka, nacho ni barua. Mshenga pamoja na kwenda kupiga domo, anakabidhi na barua ambayo itasomwa baadaye watakapoitwa baadhi ya wanandugu toka pande mbili za wazazi wa kiume na wa kike. Mara nyingi kwenye barua huwekwa pesa ambayo wanaosoma barua hugawana. Halafu baadaye mshenga mahari pia kupeleka kwa wazazi wa binti.

Watu walipoanza kujua sheria, baadhi yao walizitumia vibaya, kwani walijua ukipewa kitu bila maandishi au mtu mwingine mmoja au wawili kushuhudia, basi hata ukidhulumu huwezi kufungwa kwa sababu kunakuwa hakuna ushahidi. Hapo ndipo wengi walipodhulumiwa ardhi, mashamba, pesa na vitu mbalimbali. Ubinadamu na kule kuishi kijamaa kulianza kupungua kwa kiasi kikubwa.

Ndipo zilipoanza kuja kesi za washenga kutopeleka posa wala mahari kule walikotumwa kwa sababu mara nyingi hupewa kwa uaminifu tu. Nadhani ni hapa tulipofika ni kwamba mshenga anapopewa barua kupeleka, au mahari lazima kuwe na mashahidi wakishuhudia kwa sababu huwezi kujua nini kitatokea. Siku zote waswahili wanasema kamba hukatikia pabovu. Unaweza kumwamini mtu kwa asilimia zote, lakini huyo huyo ndiye akamwangusha.

Hapa kuna nyimbo mbili, moja ikiitwa 'Posa Nitaleta' iliyopigwa na Biashara Jazz Band utunzi wake, marehemu Juma Ubao, na 'Mshenga namba mbili', uliopigwa na Mbaraka Mwinshehe Mwaruka. Nyimbo hizi zina maudhui yanayofanana.

Kwa mujibu wake mwenyewe Ubao, wimbo huu unamhusu yeye mwenyewe ambaye alimpa rafiki yake pesa ya kushika uchumba au posa kupeleka ukweni, akiwa na nia ya kutaka kumuoa binti mmoja, lakini hakufanya hivyo, akaingia mitini. Ni mtu ambaye alikuwa analala naye chumba kimoja wakati huo wote ni 'mabachela.'

“Aaaaha, yote hupangwa na Mungu, nilitaka kumuoa, posa mali nilitoa, msichana huyu, kidogo tulipendana, nia nilikuwa nayo, ya kwamba harusi ifanyike, sijui kitu gani harusi haikuwa. Ni kazi ya Mungu, yote hupangwa na Mungu, vyote.

Hapo mwanzo nilisema, fitina za mashemeji, sasa yamenikuta, huyu mchumba wa pili.

“Kumbe mshenga katoroka, posa na mali, hakupeleka yeyeye, ohooo, nilipompa pesa hakuwepo shahidi mimi nitafanya nini yeyeye, ohoooo. Mshenga kapokea pesa zangu, hakupeleka kwa wakwe yeyeye, ohooo oooo.

“Mimi nilikwenda polisi, kumshtaki mshenga aa, polisi alisema subiri baba tutafanya uchunguzi wiki hii. Kabla wiki haijapita, polisi walinita njoo njo baba hoo, mshenga wako kakamatwa, ashtakiwe kama mwizi. Tulipofika mahakani, eee, mshenga aruka asema hakupokea pesa. Aliuliza ushahidi uko wapi eee baba eee, aliuliza maandishi yako wapi eee Makusa ha, aliuliza ushahidi uko wapi, Jeni mama subiri hii. Ani mama niteleta pesa (Jeni hooo), ooo subirini eee, subira yavuta heri, japo kuwa siyo kizito kwa macho, ai mama nitaleta posa, ooo subirini eee, ooo subirini eee.”

Wimbo huu unafanana na wa Mbaraka, ambao ulianza kutungwa kabla huo wa Juma Ubao. Mwenyewe anasema hata huo wa kwake aliuita 'Mshenga', lakini Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD), walimwambia abadilishe jina kwa sababu linafanana na jina la wimbo wa Mbaraka. Wimbo huo nao unamhusu jamaa aliyempa posa mshenga ambaye aliingia mitini. Wakwe wakawa wanauliza hivi huyu jamaa hataki mke? Aliposikia akashangaa sana na kuwaahidi atapeleka posa yeye mwenyewe. Wimbo wenyewe ni huu hapa.

“Barua nyingi zamiminika ooo, kutoka ukweni zinauliza habari za posa ooo. Vipi bwana wewe, twangoja hiyo posa mpaka sasa kimya, kama umeshindwa tuarifu upesi tumuoze mwingine.

Barua zetu zanishtua ooo, kwani siamini mnayosema nyinyi wakwe zangu, mahali nimetoa siku nyingi na kumkabidhi mshenga na pengine hajazifikisha. Toka mwezi wa juzi kama hajafika yatia wasiwasi, hili na hili sina mshenga haonekani kwenu wakwe zangu. Mwezi wa tatu, kwa nini mahari isifike na posa nimempa mshenga awaletee. Mwisho wa mwezi mimi nitafika huko, hata posa zimeliwa hiyo msijali.”

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaji, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele.
Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea na kwa nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

# Harusi Imevunjika-20

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Lakini nasikia ukawa unamnyanyasa na kumpiga mdogo wako, ukimtuhumu kuwa tuna uhusiano wa kimapenzi. Ukamfanya hata mdogo wako asiishi kwa raha hadi akaniambia atatoroka nyumbani kwenda kuishi sehemu yoyote…"

"Hayo yote mimi nimekubali, yaishe…" Akadakia.

"Hayawezi kwisha kama hakujakaa na kuyakemea haya ili iwe fundisho kwa wengine."

"Jerry, nisamehe, nataka tuishi wote, nina shilingi milioni kumi nataka nikupe ili tuanzishe biashara yoyote ile."

Ilimshtua kidogo Jerry na kumuuliza "Ziko wapi na umezipata wapi pesa zote hizo?"

"Sasa tutaongea wenyewe tukiwa pamoja, ila pesa zipo benki." Hili halikumshtua Jerry pekee, mpaka babu, mama yake na Zulfa.

Wanafahamu hajawahi kufanya biashara yoyote ile. Leo anasema ana shilingi milioni 10? Amezipataje? Jerry alihisi huenda ni maneno ya kutengeneza, ikiwa ni njia ya kumshawishi amrudie. Akashusha pumzi ambayo hakuna mtu aliyeelewa maana yake. Zulfa akamwangalia Jerry kwa jicho la utulivu zaidi.


"Huwezi kuninunua kwa vipande vya pesa. Mimi nadhani tu niongee kwa ufupi na sitorudia tena hili. Ni kwamba nakuruhusu utafute mwanamume mwingine uwe naye. Usifikiri wala usidhani kama utairudisha akili yangu nyuma."

Wakati wakiongea maneno hayo, kulisikika mlio wa gari ambalo lilisimama nje ya nyumba ya kina Vayajo. Tayari sasa kulikuwa na magari mawili kijijini hapo. Moja likiwa limepaki nje ya nyumba ya mzee Mbegu ambalo ni la Jerry. Hilo lingine hakuna aliyejua ni la nani. Lakini kitu pekee ambacho kila mmoja alijua kuwa walikuwa ni wageni kwenye nyumba ya mama Zulfa.

Aina ya gari walilokuja nalo na jinsi walivyo walionekana kabisa kuwa ni wageni waliotoka mbali. Wote walitoka na kuelekea kwenye nyumba ya mama Zulfa walipofikia.

"Karibuni wageni." Akawakaribisha mama Zulfa ingawa bado alionekana kuwa na wasiwasi kwani ni watu ambao hajawahi kuwaona hata siku moja.

"Ahsante sana." Akajibu mmoja wao kwa sauti nzito.




**"Sasa tutaongea wenyewe tukiwa pamoja, ila pesa zipo benki." Hili halikumshtua Jerry pekee, mpaka babu, mama yake na Zulfa.**

Walikuwa watatu na wote waliteremka ndani ya gari. Mmoja ambaye alionekana ni dereva, aliegemea gari. Wawili ndio waliosimama pale uwanjani, lakini mmoja ni kama alijitenga kidogo na hakuonekana kutaka kuongea kitu, akimwachia mwenzake.

"Samahanini. Sisi ni maofisa wa Polisi kutoka Makao Makuu, Dar es Salaam…" Aliposema maneno hayo kila mmoja hapo alishtuka.

Hata hivyo Jerry yeye kwa mbali kabla hata hawajasema, alipowaona tu na kuwasoma kisaikolojia alijua hawakuwa watu wa kawaida, hivyo alikuwa anasubiri nini kitazungumzwa. Hakuna aliyejibu. Ni kama kila mmoja alifungwa mdomo.

"Tumekuja hapa kwa maelekezo maalum, tunamhitaji dada mmoja anayejulikana kwa jina la Vayajo Hamisi."

Walianza kutazamana, na baada ya sekunde kadhaa, Vayajo mwenyewe alijitambulisha, ingawa kwa woga mkubwa "Ni mimi hapa."

"Basi upo chini ya ulinzi. Tunakupa muda kidogo kwa ajili ya kujiandaa ili twende Dar es Salaam."

Kulizuka taharuki kidogo, kwani mama Vayajo aliangua kilio kilichowatoa watu kwenye majumba yao na kukimbilia hapo ili kujua nini kimetokea.

"Kwani imekuwaje bwana afande?" Jerry ilibidi aingilie kati.

"Tena imekuwa vizuri sana, inaonekana wewe kidogo ni msomi. Tutaongea na wewe halafu unajaribu baadaye kuwafahamisha wazazi na wanakijiji." Akasema afande huyo ambaye sasa aliamua kutoa kitambulisho chake na kumwonyesha Jerry.

"Kama tulivyotangulia kusema, sisi ni maofisa wa polisi, tumetoka Dar es Salaam kuja kumchukua huyu dada. Si kama ana makosa, hapana, ila yuko chini ya ulinzi kwa ajili ya kwenda kusaidia uchunguzi wa wizi na utakatishaji wa pesa."

Jibu hilo lilimchanganya Jerry pamoja na hata waliokusanyika hapo. Wizi na utakatishaji wa pesa kwa mtu kama Vayajo kilikuwa kitu cha kushangaza.

"Ni kwamba tuliwakamata watu kadhaa, akiwamo mwanamume aliyekuwa anaishi naye anaitwa Jaziru kwa tuhuma hizo."

"Mhh, bado sijakuelewa afande, mwanamume aliyekuwa anaishi na huyu dada, wapi Dar es Salaam?"

"Ndiyo, wakati tunamkamata mhalifu Jaziru, tena nyumbani kwake tulifika saa nane za usiku, tulimkuta huyu dada na akajitambulisha kama mke wa mtuhumiwa."

Jerry kwa mbali alionekana kuanza kufunguka macho. Alianza kuhisi kuwa huenda Vayajo siku ya harusi alipotoroka, alikimbilia kwa mwanamume huyu anayemsema afande. Akauliza tarehe ambayo alikamatwa huyo mtuhumiwa. Alipojibiwa akapata uhakika kuwa ni kweli Vayajo alikimbilia kwa mwanamume ambaye ndiyo huyo aliyekamatwa kwa wizi na utakatishaji pesa.

Kwa upande wake hata alipotorokwa na kuanza kuhisi atakuwa ametorokea wapi hakujisumbua wala kujidanganya kuwa anatakuwa amekwenda kuishi kwa marafiki zake wa kike au kwenda sehemu kufanya biashara. Alichodhani ndicho hicho hicho ambacho sasa kinabainishwa na afande.

"Kifupi tu ni kwamba huyu dada alikuwa anaishi na mwanamume Dar es Salaam anayeitwa Jaziru. Huyu na wenzake waliiba pesa nyingi na kuzitakatisha. Tuliwakamata kama nilivyokwambia tulimkuta huyu dada. Tulimwacha pale kwa sababu sisi tulimhitaji mtuhumiwa tu. Lakini baada ya uchunguzi, tukagundua kuna miamala ya pesa kutoka kwenye akaunti ya mwanamume wake kwenda kwake kiasi cha Sh. milioni 10, ambazo zilitumwa kwa nyakati mbili tofauti.

"Awali zilitumwa Sh. milioni saba na baadaye tatu. Kama nilivyokwambia hizo zote ni pesa za wizi na utakatishaji kwa sababu watuhumiwa hao wako rumande. Tumekuwa tukiwakamata watu wote ambao akaunti zao zilikuwa zinaingiziwa pesa na watuhumiwa. Tunafanya hivyo kwa ajili ya mahojiano, uchunguzi na kujidhihirisha ili kukusanya taarifa zote na kuchuja nani alihusika na nani hakuhusika. Kama ziliingizwa tu na huyu dada hakuhusika, basi atakuwa hana kesi ya kujibu, tutamrudisha sisi wenyewe lakini kama atakuwa ameshirikiana na mwanamume wake basi atapanda mahakamani."

Mambo yamekuwa makubwa. Kila kitu kilikuwa kinamshangaza Jerry. Tarehe aliyotajiwa na askari ambayo Vayajo aliingiziwa pesa, ilikuwa ni ile ambayo alimtoroka na kwenda kusikojulikana. Hakujua kuwa zile Sh. milioni saba za mwanzo alizoingiziwa na Jaziru, ndizo zilizomtia uchizi na kuamua kutoroka muda mfupi tu kabla ya kufunga ndoa.

Sasa ndipo Jerry alipotambua kuwa kukimbiwa kule kulichangiwa kwa asilimia kubwa na pesa zile za wizi na utakatishaji kutoka kwa mwanaume mmoja asiyemfahamu, anaitwa Jaziru. Siri sasa ilikuwa imefichuka.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# DAVIDO BADO SANA KUPERUZI

MASHABIKI wa muziki wa Afrobeat, wanaendelea kumsubiri kipenzi chao mwanamuziki wa Nigeria,Davido, kurudi katika mitandao ya kijamii baada ya kuamua kukaa kimya kwa muda mrefu.

Davido ambaye alikuwa na kawaida ya kutupia kila siku matukio kadhaa katika mitandao ya kijamii, kwa muda mrefu hajaonekana tangu apate msiba wa mtoto wake mwishoni mwa mwaka jana.

Mashabiki kutoka kwenye majukwaa ya mitandao ya kijamii wamekuwa wakishiriki baadhi ya matukio muhimu ya nyota huyo.

# WILLY PAUL, BAHATI SASA KUMENOGA

WASANII maarufu nchini Kenya, Kevin Bahati na Willy Paul, hatimaye wamemaliza tofauti zao na kutangaza sasa wanaangalia mbele.

Ushindani wa wasanii hao wa muziki ni wa muda mrefu, huku ukikolezwa na mashabiki ambao wamekuwa wakimuunga mkono msanii wanayempenda.

Hivi karibuni Willy Paul, akiwa amejawa na hasira, alimkashifu Bahati na mkewe, Diana Marua, na hivyo kuzua tafrani kwenye mitandao ya kijamii.

Hata hivyo, katika mkutano na wanahabari juzi, Bahati hatimaye amesema hakuna tena ugomvi kati ya wawili hao.

"Nani alisema sijamsamehe? Sikuwahi kusema nimemkasirikia popote pale," Bahati alifafanua.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA

### MESSI KUREJEA ARGENTINA
MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi, anatafakari juu ya uwezekano wa kurejea kwenye klabu yake ya utotoni ya Newell's Old Boys. ***(UOL, via Mirror)***

### FELIX ANOGEWA CHELSEA
MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Felix, mwenye umri wa miaka 23, anataka kuufanya mkataba wake kutoka Atletico Madrid uwe wa kudumu msimu huu. ***(Fijaches)***

### GRAVENBERCH ANUKIA LIVERPOOL
LIVERPOOL inataka kumsajili kiungo wa kati wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Ryan Gravenberch (20), ili acheze sambamba na mchezaji wa England na Borussia Dortmund, Jude Bellingham (19), ambaye wanamwania. ***(Express)***

### BOEHLY AITAKA STRASBOURG
MMILIKI wa Chelsea, Todd Boehly, anaangalia uwezekano wa kuinunua klabu ya Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, iitwayo Strasbourg. ***(L'Equipe)***

### STACH AGOMBEWA ENGLAND
LIVERPOOL, Newcastle United, Tottenham Hotspur na West Ham United ni miongoni mwa klanbu za Ligi Kuu England zinazomfuatilia kwa karibu kiungo wa kati wa Mainz na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Anton Stach, mwenye umri wa miaka 24. ***(90min)***

### FRANCA KUBAKIA FLAMENGO
MATHEUS Franca ambaye alikuwa analengwa na Newcastle United amesaini mkataba mpya na Flamengo, ambao walikataa ofa ya pauni milioni 17.5 kwa ajili ya kiungo huyo wa kati Mbrazili mwenye umri wa miaka 18, Januari. ***(Sun)***

### SMALLING AGEUKA LULU
KLABU za Fulham, Everton, Leicester City na West Ham United zinamtaka mlinzi wa AS Roma na England, Chris Smalling mwenye umri wa miaka 33. ***(90min)***

### KILMAN ANUKIA NEWCASTLE
NEWCASTLE United inapanga kufanya uhamisho wa kumsajili mchezaji nyota wa Wolves, Max Kilman, mwenye umri wa miaka 25. ***(Football Insider)***

### SANTOS KUTUA GALAXY
KLABU ya LA Galaxy inamtaka kiungo wa kati wa Chelsea, Mbrazil Andrey Santos, mwenye umri wa miaka 18, baada ya mpango wao wa pendekezo la kumchukua kwa mkopo kushindikana. ***(Goal)***

### ENRIQUE ATAJWA BRAZIL
BRAZIL inaweza kumwajiri kocha wa zamani wa Timu ya Taifa ya Hispania na Barcelona, Luis Enrique, kuchukua nafasi ya Tite badala ya mwalimu wa Real Madrid, Carlo Ancelotti. ***(Fijaches)***





# UNITED KUIKABILI NEWCASTLE KIBABE

## Ten Hag asema lengo ni kuhakikisha wanapata ushindi baada ya...

**LONDON, England**

ERIK ten Hag ameionya timu yake ya Manchester United kuwa makini dhidi ya wapinzani wao, Newcastle United wanaocheza kwa staili ya "kuudhi" katika mechi ya fainali ya Kombe la EFL.

United itawakabili Newcastle katika fainali itakayochezwa leo kwenye dimba la Wembley, wakiwania taji kuu la kwanza kwa msimu huu.

Lakini Ten Hag hatarajii pambano rahisi, baada ya kutambua uchezaji wa Newcastle wakati wa msimu huu.

"Nadhani ni timu kubwa," alisema Ten Hag akiwaambia waandishi wa habari kuhusu Newcastle, ambao walitoka suluhu na United kwenye Uwanja wa Old Trafford katika mchezo wa Ligi Kuu England, uliofanyika Oktoba, mwaka jana.

"Ni falsafa ya wazi kuhusu jinsi wanavyocheza mchezo. Wanafanya vizuri sana. Ni timu inayocheza mchezo wa kuudhi kucheza dhidi ya wapinzani wao, hivyo lazima tutafute njia ya kushinda."

Alipoulizwa kama alikuwa na nia ya kuelezea Newcastle kama "ya kuudhi", Ten Hag alithibitisha na kujibu: "Wanajaribu kukukasirisha. Kwa hiyo, lazima tuhakikishe tunacheza mchezo wetu na kuzingatia mchezo wetu."

Akiwa amebanwa zaidi kuhusu suala hilo, Ten Hag aliangazia jinsi Newcastle inavyopenda kupoteza muda.

"Lazima tuufanye mchezo wetu, kwa hiyo tuzingatie kazi tunayopaswa kufanya, tuzingatie soka wakati mpira unapokuwa mchezoni.

"Ni juu ya hilo, kuwa makini kabisa na hilo na usibabaishwe na chochote kilicho kwenye uwanja.

"Tunapaswa kuzingatia kazi, kutafuta njia yetu na kutafuta wakati tunaoweza kucheza vizuri."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 490

MSHINDI WA SUPA JACKPOT YA MECHI - 13




PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MARCELO AREJEA KWAO BRAZIL



**RIO DE JANEIRO, Brazil**

MLINZI wa zamani wa Real Madrid, Marcelo amerejea katika klabu yake ya utotoni ya Fluminense, baada kusaini mkataba utakaomalizika mwishoni mwa mwaka 2024.

Beki huyo mkongwe wa kushoto, ambaye alianza uchezaji wake wa soka akiwa na kikosi cha Campeonato Brasileiro, amerejea Brazil baada ya kuwa nje ya nchi hiyo kwa zaidi ya miaka 15.

Baada ya kupitia academi ya vijana na kikosi hicho chenye maskani yake Rio de Janeiro, alianza kucheza kikosi cha kwanza mwaka 2005 na akabaki hapo hadi mwaka 2007.

Baadaye alisajiliwa na Madrid, ambapo alitumia miaka 15 iliyofuata kama mtu muhimu, na kuwa mchezaji aliyepambwa zaidi wa Los Blancos katika historia yao.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 alisaini Olympiacos ya Ugiriki Septemba mwaka jana baada ya kuondoka Santiago Bernabeu, lakini akakatisha mkataba wake wiki iliyopita.

Hilo limefungua njia ya kurejea Fluminense, ambao wanatazamia kuimarisha kikosi chao na kupita mafanikio ya mwaka jana ambapo walimaliza nafasi ya tatu katika msimamo wa Ligi Kuu Brazail.

Katika kipindi chake akiwa Madrid, beki huyo alishinda mataji 25, ikiwa ni pamoja na mataji sita ya LaLiga na matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# Busquets afunguka kuhusu Europa

**BARCELONA, Hispania**

SERGIO Busquets alikiri Barcelona "wana hasira" baada ya kuondolewa kwenye Ligi ya Europa na Manchester United, lakini amesisitiza haitaathiri kiwango chao cha kuwania taji la nyumbani.


Kikosi cha Xavi kilijikuta mbio zake za Ulaya zikifikia ukingoni msimu huu baada ya kufungwa mabao 2-1 na Manchester United mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Old Trafford, Alhamisi iliyopita.

Huku vijana wa Erik ten Hag wakipata ushindi wa jumla wa 4-3 kwenye mechi zote mbili, na kuashiria jambo lingine la kukatisha tamaa kumaliza kampeni ya Ulaya kwa Blaugrana.

Barca bado wapo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga na Busquets akigusia uchungu wa kushindwa, alisisitiza watakuwa sawa.

"Kwa upande wa roho, inauma kutolewa Ulaya," alisema akiambia Movistar+. "Tuna hasira, lakini timu inafahamu hilo linatoka wapi.

"Sisi ni wazuri kwenye ligi, lakini Ulaya tunakosa pointi hiyo ndogo. Ni lazima tutamani kushinda kila kitu. Tuko kwenye njia sahihi, na nina uhakika hii haitaleta madhara kwa timu. "



## HABARI MICHEZO

# ,825,190

# JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/02/22 | 22:45 | Preston vs Coventry | 2.46 | 3.19 | 2.70 |
| 02. 28/02/22 | 22:45 | Barrow vs Salford City | 2.46 | 3.15 | 2.90 |
| 03. 28/02/22 | 22:45 | Gillingham vs Bradford City | 2.85 | 3.15 | 2.46 |
| 04. 28/02/22 | 23:00 | Luton Town vs Millwall | 2.27 | 3.15 | 3.00 |
| 05. 01/03/22 | 19:00 | Slovacko vs Bohemians | 2.35 | 3.37 | 2.64 |
| 06. 01/03/22 | 19:00 | Farco FC vs Arab Contractors | 3.63 | 2.78 | 2.27 |
| 07. 01/03/22 | 20:00 | NK Osijek vs Hajduk Split | 2.69 | 3.11 | 2.46 |
| 08. 01/03/22 | 22:15 | FC Sion vs FC Lugano | 2.51 | 3.31 | 2.51 |
| 09. 01/03/22 | 22:15 | St. Gallen vs FC Basel | 2.26 | 3.48 | 2.70 |
| 10. 01/03/22 | 23:00 | Osasuna vs Athletic Bilbao | 2.98 | 2.98 | 2.48 |
| 09. 02/03/22 | 20:00 | Aalborg vs Viborg FF | 2.80 | 3.27 | 2.29 |
| 11. 02/03/22 | 22:45 | Royal Antwerp vs Union Saint Gilloise | 2.45 | 3.30 | 2.67 |
| 13. 02/03/22 | 23:00 | Real Madrid vs Barcelona | 2.51 | 3.34 | 2.65 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAPILI - 26/02/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:15 | 2058 | Fortuna Sittard vs Feyenoord | 6.36 | 4.67 | 1.41 |
| 14:15 | 4618 | Den Bosch vs ADO Den Haag | 3.25 | 3.56 | 2.01 |
| 14:30 | 3031 | Ufa vs Akhmat Grozny | 3.32 | 3.84 | 1.86 |
| 14:30 | 4921 | Bologna vs Inter | 4.74 | 3.61 | 1.69 |
| 15:00 | 4925 | Lorient vs AJ Auxerre | 2.12 | 3.34 | 3.29 |
| 15:30 | 1220 | Hannover vs Magdeburg | 1.91 | 3.72 | 3.47 |
| 15:30 | 1520 | St. Pauli vs Hansa | 1.75 | 3.57 | 4.36 |
| 15:30 | 2465 | Arminia Bielefeld vs Heidenheim | 2.83 | 3.23 | 2.40 |
| 15:30 | 5074 | Brugge vs KAA Gent | 2.12 | 3.53 | 3.13 |
| 16:00 | 1098 | Horsens vs Viborg FF | 3.53 | 3.63 | 1.94 |
| 16:00 | 2470 | Athletic Bilbao vs Girona | 1.67 | 3.70 | 5.00 |
| 16:00 | 4345 | Umraniyespor vs Adana Demirspor | 3.18 | 3.50 | 2.11 |
| 16:00 | 5005 | Randers vs Lyngby | 1.86 | 3.73 | 3.73 |
| 16:15 | 3572 | FC Luzern vs Grasshoppers | 1.81 | 3.77 | 3.87 |
| 16:15 | 4389 | FC Vaduz vs Neuchatel Xamax | 2.03 | 3.52 | 3.10 |
| 16:30 | 1145 | Tottenham vs Chelsea | 2.42 | 3.21 | 2.81 |
| 16:30 | 1573 | Vitesse Arnhem vs Ajax | 5.35 | 4.55 | 1.49 |
| 16:30 | 1627 | Emmen vs GO Ahead Eagles | 2.34 | 3.22 | 2.92 |
| 17:00 | 1317 | Salernitana vs Monza | 3.31 | 3.31 | 2.10 |
| 17:00 | 3157 | Clermont Foot vs Strasbourg | 2.50 | 3.10 | 2.85 |
| 17:00 | 3758 | Reims vs Toulouse | 2.08 | 3.49 | 3.24 |
| 17:00 | 5090 | Nantes vs Rennes | 3.27 | 3.27 | 2.16 |
| 17:00 | 5198 | AC Ajaccio vs Troyes | 2.22 | 3.08 | 3.33 |
| 17:30 | 1237 | SC Freiburg vs Bayer Leverkusen | 2.16 | 3.42 | 3.07 |
| 18:00 | 2417 | OH Leuven vs Royal Antwerp | 3.34 | 3.49 | 2.04 |
| 18:00 | 2429 | Copenhagen vs Aalborg | 1.36 | 4.68 | 7.77 |
| 18:00 | 3198 | Rangers vs Celtic | 3.01 | 3.37 | 2.13 |
| 18:15 | 2367 | Levante vs Lugo | 1.32 | 4.54 | 9.67 |
| 18:15 | 3638 | Celta Vigo vs Valladolid | 1.67 | 3.70 | 5.00 |
| 18:15 | 4693 | Ascoli vs Benevento | 2.34 | 3.12 | 3.01 |
| 18:30 | 1817 | Rio Ave vs GD Chaves | 2.15 | 3.23 | 3.33 |
| 18:30 | 2860 | FC Lugano vs FC Basel | 2.64 | 3.34 | 2.52 |
| 18:45 | 3612 | PSV Eindhoven vs Twente | 1.61 | 4.08 | 4.67 |
| 19:00 | 1858 | Namungo vs Geita Gold FC | 2.57 | 2.81 | 2.81 |
| 19:00 | 3611 | Besiktas vs Antalyaspor | 1.72 | 3.65 | 4.54 |
| 19:00 | 4308 | RB Salzburg vs Josko Ried | 1.17 | 6.23 | 11.42 |
| 19:05 | 5051 | Monaco vs Nice | 2.00 | 3.48 | 3.48 |
| 19:30 | 2059 | Bayern Munchen vs Union Berlin | 1.31 | 5.16 | 8.14 |
| 19:30 | 2725 | Manchester Utd vs Newcastle | 2.20 | 3.22 | 3.22 |
| 20:00 | 5031 | Aarhus vs Silkeborg | 2.25 | 3.22 | 3.12 |
| 20:00 | 5046 | Udinese vs Spezia | 1.60 | 3.83 | 5.17 |
| 20:30 | 3443 | Almeria vs Barcelona | 6.00 | 4.41 | 1.48 |
| 20:30 | 4016 | Las Palmas UD vs Ponferradina | 1.46 | 3.97 | 6.96 |
| 20:30 | 4811 | Anderlecht vs Standard Liege | 1.87 | 3.59 | 3.84 |
| 21:00 | 3445 | Pacos Ferreira vs Boavista | 2.65 | 3.05 | 2.70 |
| 21:15 | 4661 | Charleroi vs St Truiden | 2.09 | 3.38 | 3.33 |
| 22:45 | 2012 | AC Milan vs Atalanta | 2.14 | 3.32 | 3.22 |
| 22:45 | 2716 | Marseille vs Paris St Germain | 2.62 | 3.49 | 2.46 |
| 23:00 | 5793 | Sevilla FC vs Osasuna | 1.87 | 3.35 | 4.21 |
| 23:30 | 5898 | Porto vs Gil Vicente | 1.19 | 6.73 | 11.87 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# TONY AMPA MKANDA WA ABU RAIS SAMIA

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kutetea mkanda wa ubingwa wa Afrika (ABU) kwa kumchapa, bondia kutoka Afrika Kusini, Sabelo Ngabinyana, mwenyeji Tony Rashid, amesema ushindi alioupata katika pambano lililofanyika juzi anaupeleka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Tony amefanikiwa kuchukuwa tena mkanda huo katika uzito wa Super Bantam kwa pointi kwenye pambano lilofanyika Dar es Salaam, juzi usiku.

"Sabelo amenipa changamoto kubwa sana, namshukuru Mungu kwa kufanikiwa kutetea kwa mara ya tatu huu mkanda, ushindi huu sio wangu bali ni zawadi kwa mama Samia. Kupata wapinzani wakali kwangu inanipa nguvu ya kuongeza bidii katika mazoezi na kutambua namna ya kurekebisha mapungufu, " alisema Rashid.

Promota wa pambano hilo, Saada Salim, alisema kampuni yao imejipanga kuandaa mapambano mengine ya kiwango cha juu kwa lengo la kuwapa changamoto mabondia wa Tanzania.

Saada alisema wanahitaji kuona mabondia wa Tanzania wanapanda viwango kwa kucheza na wapinzani kutoka nchi zilizotuzidi.

Katika pambano lingine Emmanuel Mwakyembe alitoka sare dhidi ya Said Bwaga sawa na Oscar Richard alizipiga na Adam Mbega.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Salim Abdallah (katikati), akizungumza na wachezaji wa timu hiyo (hawako pichani), kuelekea mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Vipers FC iliyochezwa mjini Entebbe, Uganda jana usiku. Kushoto ni Mwenyekiti wa klabu hiyo, Murtaza Mangungu na kiongozi wa zamani, Aden Rage. **PICHA: SIMBA SC**

# Yanga yatamba kulinda heshima

INATOKA UK . 24

sehemu ya mashabiki wetu," alisema Kamwe.

Naye Rais wa AS Real Bamako, Fakaman Dembele, alisema wenyeji wapo tayari kwa mchezo huo na anaamini watapata ushindi licha ya kutarajia upinzani mkubwa kutoka kwa Yanga.

"Sisi ni timu kubwa katika bara la Afrika na tunacheza nyumbani kutokana na ubora wetu na jinsi tunavyowafahamu Yanga, tunawaheshimu kwa sababu wana kikosi bora na imara, lakini kwetu lazima tushinde. Tunahitaji sana pointi tatu za hapa nyumbani, kila mmoja alifadhaika sana na matokeo ya mechi yetu Jumapili iliyopita dhidi ya US Monastir tulipopata sare ya bao 1-1, naamini katika mechi hii tutashinda dhidi ya wenyeji wetu kutoka Tanzania," alisema rais huyo.

Wakati huo huo, kocha na nyota wa zamani wa Yanga, Boniface Mkwasa, amewataka wachezaji wa timu hiyo kuhakikisha hawatoi nafasi kwa wapinzani wao kutawala mpira dakika za awali.

Mkwasa alisema Yanga wanahitaji kucheza kwa tahadhari katika mchezo huo na kujilinda zaidi kwenye dakika 15 za awali.

"Kama mdau wa mpira nashauri Yanga wacheze kwa tahadhari katika mchezo huo wa ugenini, kutotumia nguvu na kutofunguka kwa haraka ndani ya dakika 15 za awali, wanatakiwa kuangalia wanawezaje kuzuia goli lisiingie mapema, halafu baadaye kasi yao ikipungua ndio wafanye mashambulizi ya kushtukiza," Mkwasa alisema.

Ushindi wa aina yoyote kwa Yanga leo unawasogeza na kuwaweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele katika mashindano hayo.

Yanga na Simba ndio wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

# Michezo

Jumapili Februari 26, 2023

Nipashe




United kuikabili Newcastle kibabe

UKURASA 21




Wachezaji wa Yanga, Fiston Mayele (kushoto) na Stephane Aziz Ki wakifanya mazoezi kwa ajili ya kuwavaa AS Real Bamako katika mechi ya hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa leo huko Mali. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga yatamba kulinda heshima

## ●●● Ni katika kusaka ushindi dhidi ya Real Bamako ili kujisafishia njia ya kutinga...

**Adam Fungamwango na Hadija Mngwai**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Bara, Yanga wanatarajia kuwakabili AS Real Bamako katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa kwenye Uwanja wa 26 Mars, Mali kuanzia saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania.

Yanga inayoshika nafasi ya pili katika Kundi D, itacheza mechi yake ya pili ugenini baada ya ile ya kwanza dhidi ya US Monastir ya Tunisia ambayo ilifungwa mabao 2-0, kabla ya kuitwanga TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), mabao 3-1 ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Matokeo ya mechi hiyo yanaweza kubadilisha msimamo wa kundi hilo baada ya mapema kuanzia saa 10:00 jioni, TP Mazembe kuwakaribisha US Monastir.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi aliliambia gazeti hili kikosi chake kiko tayari kwa ajili ya mechi hiyo, huku akiwa na matumaini ya kupata ushindi au sare na kujiimarisha katika msimamo wa kundi lao.

Nabi alisema katika mazoezi ya mwisho alikuwa akitilia mkazo wachezaji wake namna ya kumalizia kwa usahihi ili watumie vyema nafasi watakazopata hasa kwa njia ya krosi na zile ambazo wanabaki na magolikipa.

"Kitu bora ni tumetanua matumizi ya mifumo yetu, tunaweza kubadilika kutokana na mpinzani tunayekutana naye na ubora wake, hii ni faida yetu kubwa. Kitu nilichowaambia wachezaji wangu wanatakiwa kutupa heshima na thamani kwa kuendeleza kasi ya ushindi, ingawa nafahamu haitakuwa rahisi, tunapaswa kujitoa na kucheza kwa umakini," alisema Nabi.

Aliongeza mara kadhaa amekuwa akitumia mfumo wa 4-4-3 lakini wanaweza kubadilika kutokana na mchezo utakavyoendelea.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema maandalizi ya mchezo huo yamekamilika na wanashukuru kwa mapokezi mazuri waliyopata kutoka kwa mashabiki wa soka nchini humo tangu wawasili na hiyo imesababishwa na kipa wao chaguo la kwanza, Djigui Diarra na Mamadou Doumbia, kuzaliwa nchini humo.

"Timu imejizoea mashabiki, wamekuwa wakijazana kwenye mazoezi yetu kwa sababu ya Diarra na Doumbia, hivyo tunaona ni kama hatutokuwa ugenini sana, mashabiki wa wachezaji hao watakuwa

INAENDELEA UK . 23

## Ni Mshikemshike Kili Marathon leo

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

WANARIADHA zaidi ya 5,000 kutoka nchi mbalimbali duniani wanatarajia kushiriki mbio za kimataifa za Kilimanjaro (Kilimanjaro International Marathon 2023), zitakazofanyika leo kwenye viwanja vya Chuo cha Ushirika Moshi (MoCU), mkoani Kilimanjaro.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mbio hizo zinazofanyika kila mwaka kwa kuandaliwa na Kampuni ya Executive Solutions.

Meneja wa Bia ya Kilimanjaro, Pamela Kikuli, amesema maandalizi yote yamekamilika na wanawataka washiriki wote wa mbio hizo kufika mapema uwanjani ili kutimiza ndoto zao za kushindana mwaka huu.

Kikuli alisema wanafurahi kuona washiriki wa mwaka huu kutoka ndani na nje ya nchi wameongezeka.

"Tunatarajia Waziri Mchengerwa ataanzisha rasmi mbio za kilomita 42 na zile za kilomita 21, halafu yeye mwenyewe atashiriki mbio za kilomita tano ambazo zinadhaminiwa na Grand Malt," alisema Kikuli.

Aliongeza mbio hizo zilitanguliwa na maonyesho maalaum yajakulikanayo kama Kili Expo yenye lengo la kutoa fursa kwa wadhamini kuonyesha bidhaa, huduma na shughuli mbalimbali wanazozifanya kupitia taasisi zao.

"Tunatoa wito kwa washiriki wa mbio hizo kuzingatia muda, na tunawakumbusha hakutakuwa na tukio la kutoa namba au vifaa siku ya kesho (leo), washiriki watakaoshiriki ni wale waliojiandikisha kwa kufuata taratibu zote", aliongeza ofisa huyo.

Aliwakumbusha wanariadha wanaotarajia kutumia namba za miaka ya nyuma kutofanya hivyo na hairuhusiwi kutumia namba iliyoandikishwa na mshiriki mwingine.

Wadhamini wakuu wa mbio hizo ni Bia ya Kilimanjaro (kilomita 42), Tigo (kilomita 21), Granda Malt (kilomita tano) huku wengine ni TPC Sugar, Simba Cement, Kilimanjaro Water, TotalEnergies, Surveyed Plots (SPC), Kibo Palace, CMC Autobobiles, KK Security na hoteli ya Keys.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >